⁶ Sambi, íturiwa karibu nopare mivulo sita ya mawe, kila nvulo ukingira maji kiyasi ca lituru miya. Mivulo-yo wakitúmira Mayahudi wakati wa kutawada wawe swafi.⁷ Insa akiwambira maudumu ware javi: “Eyi mivulo-ji ijazani maji.” Newo wakijaza mpaka pakanywa.⁸ Ikisa akiwambira: “Sambi, tekani aba, mukampe amiri wa jambo-ri.” Ewo wakiteka, wakuka wakimpa.

⁹ Amiri wa jambo ire akiyeza maji átatadiwi vinyu are, fala ejewe kawatekire maji are. (Ila maudumu ware wakijiwa konta ndi watekire.) Noparepare, amiri wa jambo ire akitumiza kumwita mwénye harusi,¹⁰ akimwambira: “Wanu piya wa-zowerera kwanza kuudumu vinyu ngema, ikisa wakinywa pakulu ndi paiudumiwa

† 1:51 Ona Mwanzo 28:12. Kamba Mwenyezimungu asowera javi ka javi na Yankubu julu ya malaika, novyo-novyoní Mwenyezimungu asowera javi-ka-javi na Insa. *

* 2:14 Evi vikuna nluwani mwa wanu Sawari-Mayahudi nNyumba Takatifu.

† 2:14 Ikisakikiana kukakanya nzuruku nNyumba Takatifu konta wanu wakisakula kutumira nzuruku kuwauza manyama ipate wawatendere kafara. † 2:16 Mana ake: Insa epa akisowera kuhusu mahala páturiwe kuntukuza Mwenyezimungu wanu Sawari-Mayahudi. Ona Zagariya 14:21. § 2:17 Ona Zaburi 69:9. * 2:21 Maria ake ndi kuwa wamulaya, fala suku ya tatu afufuka. Kwa javyo ndi kulamusua upya nyumba ya mwiri wake. † 2:22 Zaburi 69:9 kambiriwa aya 2:17 julu.

vinyu sairevy-a-yi. Fala umwe mutula vinyu ngema mpaka sambi-pa!”

¹¹ Insa katenda eyi alama ya maajuya akwanza-ya kaya ya Kanaa porovinsiya ya Galileya. Kwa javyo ndi yvolute utukufu wake, ndimana wanafunzi wake wakinkubali.¹² Bandi ya evi, Insa akilongozana na mamaye, wanduze, pamoja na wanafunzi wake, wakiteremukira kaya ya Kafarnaumu, wakikala noko fala awekare suku nyingi.

Insa aswafi Nyumba Takatifu

¹³ Suku ya Pashukwa íkiwa karibu-karibu, suku ya sherehe ya Mayahudi, ndimana Insa kákwerwa Yerusalem. ¹⁴ Akiwasingana wanu nluwani nNyumba Takatifu* wakiúzanya ng'ombe, makondoo, na mapomba, na wengine wekáre mmameza wakikakanya mizuruku†.¹⁵ Iye akitwala nzizi akipikisa nkajju, akiwatuwisa wanu piya nluwani mure, pamoja na makondoo na ng'ombe. Mizuruku ya wanu wakikakanya ware akefya coro-coro-coro, na meza zawo akipindula pindu-pindupindu.¹⁶ Akiwambira wanu wakiúzanya mapomba ware javi: “Umwe, evi vinu-viaya lavyani-pa! Nyumba ya Baba-ysi mutwakalija kutenda bazari‡?”

¹⁷ Wanafunzi wake ware wakumbukira vyaandikiwe Mandiko Matakatifu§ kuwa javi: “Wivu wautendera Nyumba yako uwa kamba moto vyaunoca.”¹⁸ Sambi, Mayahudi wandairi, wamba: “Uwe uri na mamulaka yakutenda evi vinu-vi, ukolota alamani?”¹⁹ Insa akiwajibu, akamba: “Dangulani Nyumba Takatifu-ji, kwa muda wa suku natu nilamusá!”²⁰ Kwa javyo Mayahudi wakinjibu: “Eyi Nyumba-ji ijengiwa myaka arubaini na sita. Uwe kwa muda wa suku natu basi ulamusaja?”²¹ Fala iye akamba mwiri wake mwanyewe.*²² Ndimana, paafufuke ka wafwi, wanafunzi wake wakumbukira kuwa iye kásema novi,

* 2:17 Ona Zaburi 69:9. * 2:21 Maria

† 2:22

basi wakikubali Mandiko Matakatifutu pamoja na usemi waasowere Insa.

Insa akwijiwa mawazo a wanu piya

²³ Insa paakiwa Yerusalem kusherehe ya Pashukwa, wanu wengi wankubali iye[‡], kwa kuwona alama za maajuza zaakitendanga iye. ²⁴ Fala Insa mwanyewe ewo aawakubalire, konta piya wanu akiwejiwa. ²⁵ Aakinsakula munu wakumwámbira ewo cawawaza, konta iye akijiwa sana-sana mawazo a mwanadamu.

3

Insa asowera na Nikodemu kuhusu mainsha mapya

¹ Ákiwapo mwananlume mmoja Nfarizeu ákitiwa Nikodemu, iye ndi ákiwa nlongozi mmoja wa Mayahudi*. ² Kwa suku moja usiku, koka ka Insa, akimwambira: “Mwanlimu, tikwijiwa kuwa uwe kuwa mwanlimu kuperekwiwa na Mwenyezimungu. Kamana aapo akidiri kutenda alama za maajuza zautenda-zi ikiwa munu-yo áari upande wa Mwenyezimungu.” ³ Insa akinjibu akimwambira javi: “Nukwambira kweli-kwelini kuwa ikiwa munu aapongoriwe mara yapiri†, awona futi ufalume wa Mwenyezimungu.” ⁴ Nikodemu akindairi: “Munu ari nkulu, aludira kupongoriwa mwaja? Vikidirika kulidira mmatumbo mwa mamaye apongoriwe tena?” ⁵ Insa akinjibu: “Nukwambira kweli kuwa munu sáapongoriwe kwa maji na kwa Roho wa Mwenyezimungu, iye engira muufalume wa Mwenyezimungu.” ⁶ Apongóriwe na mwiri ndi mwiri, na apongóriwe na Roho wa Mwenyezimungu ndi roho.

⁷ Uwe usishange vyanukwambire kuwa ibidi mupongoriwe mara yapiri. ⁸ Mepo ivungira kaisaka konse, na shauti yake usikira, fala awijiwa ndeyi kailawirira wala kayukirira. Ndi namuna moja noyo munu wakupongóriwa julu ya Roho wa Mwenyezimungu‡. ⁹ Nikodemu akindairi, akamba: “Vinu kamba-vyo viwaja?” ¹⁰ Insa akinjibu akimwambira javi: “Uwe kuwa mwaniimu nkulu wa walzraeli. Evi vinu vi-

‡ 2:23 Kigeregu: “Wanu wengi wakubali zina rake.” *

† 3:3 Kigeregu: au “aapongoriwe binguni”. ‡ 3:8

mwanyewe. * 3:14 Ona Isabu 21:9. † 3:15 Mana ake: Insa epa akiramba iye mwanyewe paasaka kuja kulamusiwa pansalaba. ‡ 3:18 Kigeregu: “aaminire zina ra Mwana mmoja tu basi wa Mwenyezimungu”.

aavikwerera sababuni? ¹¹ Nukwambira kweli kuwa vyatijiwa tikwereza, na vyatiwonire tankulavya ushahidi, fala ushahidi wetu umwe amukubali. ¹² Ikiwa nukwambiranu vinu vikuna mulumwengu-mu amunikubali, futi nukukwambiranu vyabinguni mukubalija? ¹³ Aapo akweríre kuka binguni sairi Binadamu wa Binguni§ esíke kulawa binguni. ¹⁴ Kamba Musa vyanlamuse nyoka nlanga*, na visakikana novyo kulamusiwa Binadamu, ¹⁵ ipate kila mwenyé kumwamini onse apate mainsha a milele.[†] ¹⁶ Kamana Mwenyezimungu kawapenda wanu mulumwengu javi: kawagabizi Mwanawé mmoja noyo tu basi, ipate kila mwenyé kumwamini asipoteye nifululu fala awe na mainsha a milele.

¹⁷ Konta Mwenyezimungu aampereke Mwanawé mulumwengu-mu kuwalamula hukumu wanu, ila kampereka ipate wanu wapate kuvuka julu yake iye. ¹⁸ Amwámini aalumuriwa hukumu, ila saamwámini kesa kulamuriwa hukumu futi, konta aamini caari Mwana mmoja tu basi wa Mwenyezimungu‡. ¹⁹ Na javi ndi namuna vyakujire kulamuriwa hukumu, kwa kuwa ija nuru mulumwengu-mu, fala wanu wapenda pakulu kisi koliko nuru konta vitendo vyawo vya ubaya. ²⁰ Kamana kila munu aténda vitendo vya ubaya inkima nuru, na aaja pairi nuru, ipate visiwoneke vitendo vyake. ²¹ Fala ire aténda vitendo vyakweli akuja pairi nuru, ipate wanu wawone kuwa vitendo vyake kankutenda julu ya Mwenyezimungu.”

Yahaya mwenyé Koza akwamba kuwa Insa ndi bora

²² Bandi ya evi, Insa pamoja na wanafunzi wake wakija inti ya Yudeya. Akikalawo nokure, akozanga wanu. ²³ Yahaya novyo akozanga wanu Ainoni karibu ya Salemu, konta noko ákiwapo maji mengi. Wálkjanga wanu, wakoziwa. ²⁴ Epo Yahaya saanamba kufungiwa nkalaboshu.

²⁵ Sambi, wanafunzi wa Yahaya na Yahudi mmoja wakanza kukaidiyana kuhusu kutawada. ²⁶ Ewo wakija ka Yahaya,

* 3:1 Nikodemu ákiwa nlongozi, nkati ya Baraza ya Milandu.

§ 3:13 Insa epa akiramba iye Ona novyo Yahaya 1:13.

3:14 Ona Isabu 21:9. † 3:15 Mana ake: Insa epa akiramba iye mwanyewe paasaka kuja kulamusiwa

wakimwambira: "Mwanlimu, ire waúkiwa nawo ng'ambu nyengine ya muto wa Yordani, noire waukfílavya ushahidi wake ire, iye kankoza wanu, na piya wanu wankuka kwake iye!"²⁷ Yahaya akijibu, akamba: "Hapana munu apáta kinu sesusirini kulawa binguni."²⁸ Anta nomwe-mwe muwa mashahidi wangu yyanambire omi: 'Omi siri Almasihi, ila ndi niperikiwe kábula ya kuja iye.'²⁹ Ári na mwari-harusi ndi mwenye-harusi, fala rafiki wa mwenye-harusi ndi arípo epa, na anzikíra akwu radi pakulu kwa sababu ya shauti ya mwenye-harusi. Kwa javyo, radi yangu itímu.³⁰ Lazima iye awe bora pakulu, ubora wangu upunguke."

Alawíre binguni atipa mainsha meema

³¹ Yahaya akizidi kusema, akamba: "Alawíre julu binguni ndi bora koliko piya. Munu wa mulumwengu-muwa mulumwengu nomu, na asowera kiulumwengu. Alawíre binguni ndi bora koliko piya." ³² Asikíre na awoníre eyvo kankulavya ushahidi, fala hapana akubali ushahidi wake. ³³ Novyo-sivyo, mwenyé kukubali ushahidi wake akwakikisha kuwa Mwenyezimungu ndi mwenyé ukweli. ³⁴ Konta aperékiwe na Mwenyezimungu asowera usemi wa Mwenyezimungu, kamana iye akumpa Roho bila kipimo. ³⁵ Baba ampenda Mwanawe na piya vinu kangabizi mmakono mwake. ³⁶ Ankubali Mwanawe onse kanawo mainsha a milele. Fala saansikiriza Mwanawe onse aapata mainsha, ila nyongo ya Mwenyezimungu ikuwa julu yake iye."

4

Insa asowera na mwanamuka wa Samariya

¹ Mwenye Insa, pejiwe kuwa Mafarizeu wásikira kuwa iye kankoza wanu wengi na ákiwa nawo wanafunzi zaida ya Yahaya,² (ingawa Insa mwanyewe siakoza, ila wakoza ndi wanafunzi wake),³ iye akilawa Yudeya, akiludira tena Galileya. ⁴ Ikimbidi apite Samariya. ⁵ Basi, akija ire mpaka kaya moja ya Samariya yakwitiwa Sikari, karibu na uweru Yankubu wampere mwanawe Yusufu. ⁶ Noparepare úkiwepo nrímbu waasimbire Yankubu. Ndimana, Insa kwa

kuwa kasokera na safari yake, akikala pannrimbu nopare. Nowo wakati-wo íkiwa karibu ya aduhuri.

⁷ Noparepare, akija mwanamuka mmoja nSamariya kuteka maji. Insa akimwambira: "Nunu, nimereni maji ninywe."⁸ (Epo iri wanafunzi wake woka kaya ulu kuuza cakurya.) ⁹ Mwanamuka nSamariya ire akinjibu: "Umwe muwa Yahudi, omi niwa nSamariya. Munilebelaja maji a kunywa?" (Akisema javyo kamana Mayahudi na waSamariya awakipatana.) ¹⁰ Insa akinjibu, akimwambira javi: "Kamba ukijiwa uwezo wa Mwenyezimungu, na ari kukulebelaja maji a kunywa-yo, uwe ndi ukisaka kunkelabela, na iye nanga kakupa maji a mainsha ako."¹¹ Iye akimwambira: "Mwenye, umwe amuna ndoo, na nrímbu-wu wica pakulu. Sambi maji akunipa mainsha-yo, musaka kupata ndepi?" ¹² Ewu nrímbu-wu katipa babu yetu Yankubu. Wákinywanga iye na wanawe pamoa na mifuwo yake. Sambi, uwe kunzaidi iye?"¹³ Insa akinjibu, akamba: "Eya maji-ya anywa onse iludira kunkola nyotwa tena."¹⁴ Fala munu akinywa maji animpa omi, ainludira futi kunkola nyotwa kwa milele. Kwasa javyo, maji animpa omi, kwake iye antadukira kuwa nviriro wakububuka mainsha a milele."¹⁵ Mwanamuka ire akimwambira: "Mwenye, nimere noyo maji-yo ipate isinikore nyotwa tena, wala nisije epa tena kuteka maji!"¹⁶ Insa akimwambira: "Uka ukamwite nlumako, muje onse."¹⁷ Mwanamuka ire akinjibu, akamba: "Omi sina nlume."

Insa akimwitikizira: "Kusowera sana kwamba: 'Omi sina nlume'.¹⁸ Kwa kuwa úkiwa nawo walume watanu. Na nlume waúri nawo sambi-yo siyo nlumako. Epo kusowera kweli yako!"¹⁹ Mwanamuka ire akimwambira Insa: "Mwenye, omi niwona kuwa uwe kuwa nabii!"²⁰ WaSamariya wababu zetu, pawakabudu ndi nowu mwango-wu. Fala umwe Mayahudi mukwamba kuwa mahala wanu pawajuzi kwabudu ndi Yerusalemu."²¹ Insa akimwambira: "Nunu, namini omi vyankwambira-vi: ukuja kufika wakati wakuwa ewu mwango-wu wala Yerusalemu amuja kumwabudu Baba.

§ 3:29 Mana ake: Insa ndi mwenye harusi, mwari harusi ndi wenye kumwamini Insa, na rafiki wa mwenye harusi ndi Yahaya mwenyé Koza.

²² Umwe waSamariya mumwabudu nlungu samumwijiwa. Ila ofwe Mayahudi Nlungu watimwábudu timwijiwa, konta kuvushiwa kulawa ka Mayahudi. ²³ Fala wakati wankufika, na kweli epa ufika futi, ware wamwábudu ka ukweli wamwabudu Baba kwa roho, wakifulata ukweli. Kamana Baba nowo ndi wawasakula wamwabúdu iye. ²⁴ Mwenyezimungu ndi roho. Basi wenye kuntuza iye wajuzi wantukuze kwo roho, wakifulata ukweli.” ²⁵ Mwanamuka ire akilawa akamba: “Omi nukwijiwa kuwa Almasihí akuja. Na akija, atambira vinu piya.” ²⁶ Basi Insa akisema: “Omi-pa ndi noyo-noyoni, omi niri kusowera nawe-mi.”

²⁷ Kwa noure wakati ure, wanafunzi wa Insa wakiludi, washanga kunsingana Insa akipakanira na mwanamuka ire. Falakini anta mmoja andairire: “Usakulani-pa?” wala “Mbaná kwankusowera naye?” ²⁸ Ikisa, mwanamuka ire akasa nkanfú wake ure nopare, akiludira ukaya, akuka akiwerezwa wanu: ²⁹ “Tukeni mukammone munu anifafanurile piya vyanitendire. Fala noire si Almasihí?” ³⁰ Basi wanu ware wakilawa nkaya mure, wakuka mpaka kaakiwa Insa kure.

³¹ Paalawire mwanamuka ire, wanafunzi ware wakinlebelá Insa: “Mwanlimu, iryani ciwa conse-ci.” ³² Fala iye kawambira: “Omi nirya cakurya umwe samwijiwa.” ³³ Kwa javyo, wanafunzi ware wanza kudairiyana watupu: “Fala aapo ajire nawo cakurya akimpa?” ³⁴ Insa akiwambira: “Cakurya cangu omi ndi kutenda vyaasaka Mwenyezimungu anipereke, na kutimiza canitumiwe kutenda. ³⁵ Umwe musoweranga javi: ‘Ibaki tena myezi mine kufika wakati wa mavuno’, sinovsky? Fala omi nukwambirani: fungulani maso, munang’ani ze mamasamba-mo konta mbeyu piya zitokota, zisaka kuvuniwa.* ³⁶ Mwenyé kuvuna kapata nshahara wake futi, na akusánya visumo apata mainsha a milele. Kwa namuna-yi, nyvari pamoja na nrími piya watanderana radi. ³⁷ Konta ewu usowezi-wu wakweli: ‘Mmoja ndi avýála na mwengine ndi avúna.’ ³⁸ Omi nukuperekani umwe muvune camutowire kukola kazi. Wengine wanza eyi kazi-yi, umwe mwankufaika ewo caanzire kutenda.”

* 4:35 Akiwamba wanu wákiwa tayari kwingira mainsha mapya kunfulata iye.

³⁹ WaSamariya wengi wakikálanga kaya ulu ire wankubali Insa julu ya ushahidi wereze mwanamuka ure akamba javi: “Iye kanifafanurira omi piya vyanitendire!”

⁴⁰ WaSamariya pawajire, wakintafadali kuwa wekare nawo. Basi Insa akikalá nawo suku mbiri. ⁴¹ Na wengi wawenye tena wankubali Insa julu ya usesi wake iye mwanyewe. ⁴² Ewo mwanamuka ire wakimwambira javi: “Ataminiire kwa sababu vyausowere uwe basi, kamana nofwe wanyewe tinsikira. Epa tijiba kuwa eyu kweli-kwelini ndi Nvushi wa mulumwengu-mu.”

⁴³ Bandi ya suku mbiri zekare zire, Insa akilawa akiludira Galileya. ⁴⁴ (Kusema kweli, Insa mwanyewe kálavya ushahidi wakuwa aapo nabii anta mmoja wakwinshimiwa kwawo.) ⁴⁵ Paafikire Galileya, waGalileya wampokerera sana-sana, kamana wâwona piya vyaatendire Yerusalem pasherehe ya Pashukwa. Kamana ewo novyo woka noko.

Alama yapiri yolota vyaári Insa: amponesa mwana wa nkolakazi maalumu

⁴⁶ Sambi, Insa akiludira tena Kanaa porovinsiya ya Galileya, kaya yaâtaduse maji akitenda vinyu. Kaya nyengine, Kafarnaumu, ákiwapo nkolakazi maalumu wa nfalume, mwanawé ákiwa nlwere. ⁴⁷ Nkolakazi ire, paasikire kuwa Insa kalawa Yudeya kafika Galileya, akipita akin-sakula. Nakummona akintafadali pakulu pawenye akamba: “Tuke ukamponese mwanangu, iye kawa karibu kufwa!” ⁴⁸ Insa akimwambira javi: “Ikiwa amuwonire alama na maajuza, amushubutu futi kukubali.” ⁴⁹ Nkolakazi ire akijibu: “Mwenye, tuke onse sambi-pa, mwanangu saanamba kufwa.” ⁵⁰ Insa akimwambira: “Uka, mwanawo-yo apona!” Mwananlume ire akikubali usowezí wa Insa ure, akiludira kwawo.

⁵¹ Munjira paakteremukira kwawo, akisimanana na watumisi wake wakimwinza, wakimwambira wakamba: “Mwanenu kapona, kawa hai!” ⁵² Iye kawadairi: “Mwanangu kapona wakatini?”

Ewo wakinjibu: “Ijana, ‘uma ora’, homa ndi paimpitire.” ⁵³ Wawa ire kejiwa kuwa kweli-kwelini mwanawé kapona noure wakati wambiriwe na Insa ure akamba javi: “Mwanawo kapona!” Kwa

javyo, iye pamoja na wajamaa zake piya wakimwamini Insa.⁵⁴ Na eyi iwa ndi mara yapiri Insa yaatendire alama ya matajabisa paalawire Yudeya akija Galileya.

5

Alama yata tu yolota vyáári Insa: am-ponesa kitewe

¹ Bandi ya evi, rikiwapo jambo ra Mayahudi, Insa akikwera akuka Yerusalemu. ² Sambi, Yerusalemu nokurekure, karibu ya nryango wakwitiwa “Nryango wa Makondoo”, íkiwapo tanki nkiebraniya wakita “Betizata”, noyo íkiwa na vitololo-vito, ³ Nkati ya evyo vitololovo, wákiwapo wanu wengi walwere: wanu sawawona na wakuremala na vitewe.

⁴* ⁵ Nopo ákiwapo mwananlume mmoja kálwala myaka talatini na minane. ⁶ Insa paammonire aritandikire pansi, na kwa kwiija kuwa ákiwapo kure myaka mingi yawenye, kandairi: “Usaka upone?”

⁷ Nlwere ire akinjib: “Mwenye, maji-ya paaguburiwa, sina anta munu wakunauni kuningiza ntanki-mu. Panikenkeza kwingira ponse, mwengine arefyia omi san-inamba.” ⁸ Insa akimwambira: “Lamuka! Sukula nanga yako-yo, wenende!” ⁹ Kwa mpunde noure, mwananlume ire akipona, akitwala nanga yake ire, akenenda mwanyewe gidi-gidi-gidi.

Suku yaakunire eya maajuza-ya íkiwa sabadu[†]. ¹⁰ Ndimana walongozi wa Mayahudi wakimwambira mwananlume aponesiwe ire: “Uwe, rero suku ya sabadu! Siyo shariya kusukula nanga yako-yo.”

¹¹ Fala iye akiwajib: “Mwananlume aniponese omi ndi vyaanambre, iye kanambira: ‘Sukula nanga yako-yo, wenende.’ ” ¹² Ewo wakindairi: “Noyo ak-wambire: ‘Sukula nanga yako wenende-yo’, nani?” ¹³ Mwananlume aponesiwe ire aamwijiwe mununi, kamana Insa kalainika, kamana noparepare wákiwapo wanu wengi wawenye. ¹⁴ Airini Insa akisimanana naye tena noire munu ire kuluwani ra Nyumba Takatifu, akimwambira: “Wona, uwe kupona! Usikore tena dambi ipate cisukukune kinu cakofya pakulu!”

* 5:4 Eyi aya-yi aipo nkati ya mandiko andikiwe sana-sana. awakijuji kukola kazi. † 5:9 Sabadu íkiwa suku takatifu ya Mayahudi wanu haki ya Mwenyezimungu kutenda kazi daima.

¹⁵ Ikisa akilawa mwananlume ire, akanza kuwambira walongozi wa Mayahudi: “Insa ndi aniponese.” ¹⁶ Ndimana Mayahudi wakanza kunlumbata Insa kwa kuwa kâtenda evi vinu-vi suku ya sabadu. ¹⁷ Fala Insa akiwajib, akamba: “Mpaka rero Baba wangu daima-zi kankukola kazi, nnomi novyo nankukola kazi‡.”

¹⁸ Insa, kwa sababu ya kwamba javire, walongozi wa Mayahudi warimbisa mpango wakunsakula wamulaye. Aiwere kwa sababu ya kutupa shariya ya suku ya sabadu noyo tu basi. Ciwakimire pakulu ndi kwa iye kâmba Mwenyezimungu ndi wawaye-wawayeni. Kwa namuna-yi, akiritula kuwa sawa-sawa na Mwenyezimungu.

Mwenyezimungu mammulaka ake akumpa mwanawé Insa

¹⁹ Insa akikola kuwajibu akamba: “Omi nukwambirani kweli kuwa Mwana aatenda kinu cakuwaza mwanyewe ila atenda caammonire wawaye akitenda. Kamana Baba caatenda conse, Mwana neye atenda noco.

²⁰ Kweli, Baba ampenda Mwanawé na piya vinu vyaatenda, amolotera. Visitoshe, vinu vikulu-vikulu vya matajabisa vyakupunda evi akuja kumolotera ipate piya-mwe mutajabu. ²¹ Kamba Baba vyawalámusa wafwi kuwapa mainsha, Mwanawé novyo akumpa mainsha waansaka onse. ²² Kusema kweli, Baba aanlamula munu, ila kulamula piya kangabizi Mwanawé, ²³ ipate wanu piya wansifu Mwanawé kamba vyawansifu Baba. Ire akatála kunsifu Mwanawé, novyo kankukatala kunsifu Baba ampereke iye.

²⁴ Omi nukwambirani kweli: asikíriza usemi wangu onse na amwáminni anipereke omi, kanawo mainsha a milele. Iye oka kulamuriwa, ila katupa kifo, kengira futi mmainsha a milele.

²⁵ Omi nukwambirani kweli kuwa ukuja kufika wakati, na ufika futi, wafwi wakuja kusikira shauti ya Mwana wa Mwenyezimungu, na wája kusikira-wo wainshi. ²⁶ Kamana, kamba Baba vyaári nawo mainsha iye mwanyewe, iye novyo kampa mainsha Mwanawé awe nawo iye mwanyewe. ²⁷ Na kampa Mwanawé

† 5:9 Sabadu íkiwa suku takatifu ya Mayahudi wanu haki ya Mwenyezimungu kutenda kazi daima.

mamulaka a kulamula konta iye ndi Binadamu wa Binguni.

²⁸ Musitajabu kukuna kinu kamba-ci, kamana ufika wakati wakuwa piya wari mmakaburi wasikira shauti yake, ²⁹ na wakuja kulawa. Watendire meema wafufuriwa wawe na mainsha, na watendire mabayá wafufuriwa wakahukumiwe.”

Ushahidi kuhusu Insa

³⁰ “Omi sitenda kinu mwanyewe. Nilamula kamba vyanisikira. Kulamula kwangu ndi ka shariya, konta sitenda vyanisaka omi, ila vyaasaka ire anipereke omi.

³¹ Nikilavya ushahidi kuhusu omi mwanyewe, ushahidi wangu auna faida. ³² Fala kawapo mwengine alávyá ushahidi kuhusu caniri omi, Nukwijiwa kuwa ushahidi walavya kuhusu omi-wo ndi kweli. ³³ Umwe muwaperekwa wanu ka Yahaya kukudairani, na iye kalavya ushahidi kuhusu ukweli. ³⁴ Kweli, omi sipokerera ushahidi wa wanadamu, ila evi vinu-vi nukwambiraní ipate muvushiwe.

³⁵ Yahaya-yo ákiwaka kamba mwenge vyauwaka ukimwarika. Umwe nlangaza wake mutendera radi muda aba tu basi.

³⁶ Fala ushahidi wangu nkulu koliko wa Yahaya, kamana vinu Baba vyanamurire kutenda, novyo-novyoní ndi vyanitenda, vikolota ushahidi kuwa niperekwa na Baba. ³⁷ Baba anipereke omi, neye-neyení alavyanga ushahidi kuhusu omi. Shauti yake tangu amunamba kunsikira, wala umbo wake amunammona. ³⁸ Ussemi wake auri pamoa nomwe kamana amunkubali wamperekere iye. ³⁹ Mandiko Matakatifu mutunza sana-sana konta mudaniza kuwa nkati yawo mupata mainsha a milele. Noyo Mandiko-yo alavya ushahidi kuhusu omi! ⁴⁰ Fala narero, amusaka kuja kwangu omi kupata mainsha.

⁴¹ Sipokerera kutukuziwa ka wanadamu.

⁴² Fala nukwijiwa namuna yenu, kuwa nkati yenu amuna pendo ra Mwenyezimungu.

⁴³ Omi njia mulumwengu-mu kwa zina ra Baba wangu, fala amunipokerere. Ila akija mwengine wakulavya ushahidi wake mwanyewe, iye mumpokerera. ⁴⁴ Umwe íri mupokerera kusifiyana watupu, amuyerera kupata kusifiwa na Nlungu mmoja tu basi, mukubalija?

⁴⁵ Musidanizire kuwa nukuka kukwerezani ka Baba. Kawapo wakuka

kukwerezani umwe ka Baba, ndi Musa, wamuntumaini umwe. ⁴⁶ Munankubali Musa, nnomi nanga munikubali, kamana kandika kuhusu omi. ⁴⁷ Fala ikiwa vyaandike Musa amukubali, futi usemi wangu mukubalija?”

6

Alama yaane yolota vyaári Insa: akuvwisa cakurya ciwatosha wanu

¹ Bandi ya evi, Insa kalawa, kaloka ng'ambu nyengine ya Tanda ra Galileya, zina rengine ra tanda-ro Tiberiya. ² Wanu wengi wakinfulata konta wâwona alama zake za maajuba zakuwaponesa walwere.

³ Insa akikwera pamwango, akikala nopo na wanafunzi wake. ⁴ Pashukwa, suku ya sherehe ya Mayahudi, íkiwa karibu.

⁵ Insa kwefya maso, kawona kundi ra wanu wengi wakija karibu yake, ndimana akindairi Filipi: “Cakurya cakuwatosha ewa wanu-wa tisaka kuuza ndepi?” ⁶ Kandairi javyo kwa kunyerera tu basi, kamana caakisaka kutenda, akijiwa mwanyewe.

⁷ Filipi akinjibu: “Jarajara miyateni za parata aziuza mikate yakuwatosha, anta kila munu apate kipande kimoja-kimoja.”

⁸ Mwanafunzi wake mmoja wakwitiwa Andere, nyenyeeye Ansumani Peduru, akamba: “Ona, kawapo-pa nnemba mmoja ári nawo mikate mitanu ya tirigu na inswi mbiri. Fala viwatoshwa wanu wengi kamba-wa?” ¹⁰ Insa akiwambira wanafunzi wake ware javi: “Wambireni wanu-wo wekare.” Nopare mahala pare íkiwapo minyani mingi, basi piya ware wakikala bunga-bunga-bunga. Jumula ya wanu ware kuwalangala wanawalume tu basi wákiwa alufu ntanu. ¹¹ Basi Insa akitwala mikate ire, akinshukuru Mwenyezimungu, ikisa akanza kuwatongera wanu wekare ware. Inswi zire novyo akiwatongera, wakipata kamba vyawakisaka. ¹² Bandi ya kwikuta piya wanu ware, Insa akiwambira wanafunzi wake ware, akamba: “Vipande vibakire-vyo, lokoterani pamoa tuke, anta kipande kimoja cisipoteye.” ¹³ Basi ewo wakilokotera vipande vya mikate mitanu vyawátafune wanu vikibaki vire, vikijala vikalala kumi na viwiri. ¹⁴ Wanu ware, pawawonire alama yaatendire Insa ire, wakamba: “Kweli-kwelini, nabii akirindiriwa kuja mulumwengu-mu ndi

noyul!”¹⁵ Insa kejiwa kuwa wákiwa tayari kuja kunkola makunje, wantawaze kuwa nfalume. Ndimana akilawa tena yeka yake, akiludira kumwango.

Alama yatanu yolota vyáári Insa: akwennenda julu ya maji

¹⁶ Paifikire jironi, wanafunzi wa Insa wakiteremukira kutanda.¹⁷ Wakingira mungalawa, wakilokera Kafarnaumu. Juwa riswa kunja kwinukala pi, na Insa akiwa saanamba kuja pawákiwa pare.¹⁸ Ntanda mure mutimbuka kwa kuwa ikivunga mepo nydingi ti-ti-ti.¹⁹ Wanafunzi ware, pawakivuta magasiya kitambo ca kilometuru ntanu au sita, noparepare wammona Insa akiija akenenda julu ya maji, akifika karibu ya ngalawa ire! Ewo wakisusuka!²⁰ Fala Insa akiwambira: “Ndumi! Musope kinu!”²¹ Basi, wakisaka kumpokerera mungalawa mure. Kwa mpunde noure, wawona wári nlufuko kaya yawakuka ire.

Insa ndi nkate wa mainsha

²² Subuu yake, wanu wabakire ng'ambu nyengine ya tanda ire, wawona kuwa ibaki ngalawa moja tu basi. Ewo wejiwa kuwa mungalawa mure Insa eengire nawo pamoja na wanafunzi ware engire nawo, walawa yeka yawo.²³ Mahala pawátafunue wanu mikate bandi ya Insa kushukuru pare, karibu pake zikija ngalawa nyengine za Tiberiya.²⁴ Wanu ware, pawejije kuwa Insa na wanafunzi wake awapo pare, wakingira mmangalawa mwawo, wakuka Kafarnaumu kunsakula Insa.

²⁵ Pawansingane ng'ambu nyengine ya ntanda ire, wakindairi: “Mwanlimú, epa kufika rini?”²⁶ Insa akiwajibu, akamba: “Omi nukwambirani kweli kuwa munisakula siyo kwa kuwa muwona alama mojawapo, ila kwa kuwa mutafuna mikate mwikuta.”²⁷ Musikore kazi kwa anzima ya cakurya camwéfyá kunundu, ila shugulikirani cakurya cukupani mainsha a milele, caakupani Binadamu wa Binguni. Kamana ndi noyo-noyoní apewe na Mwenyezimungu Baba alama yakwakikisha.”²⁸ Ikisa wanu ware wakindairi: “Tikitenda kazi za Mwenyezimungu, tíjuzi titende kinani?”²⁹ Insa akiwajibu,

akamba: “Kazi za Mwenyezimungu ndi javi: munkubali waampereke iye.”³⁰ Kwa javyo, wandairi: “Alama yautenda tiwone tukukubali, kinani? Kwankutenda kinani?³¹ Babu zetu wárya nlanga mikate yakwitiwa maná. Kamba vyavyändikiwe mMandiko*: ‘Iye mikate ya mbinguni kawapa warye.’”³² Insa akiwambira tena: “Nukwambirani kweli kuwa akupereni mikate ya mbinguni siyo Musa. Ila Baba wangu ndi akupani mikate yakweli ya mbinguni.³³ Kamana cakurya ca Mwenyezimungu ndi ire esuke binguni, awápa mainsha wanu wa mulumwengu.”³⁴ Wamwambira: “Mwenye, noyo mikate-yo, tipe daima!”³⁵ Insa akiwambira: “Omi ndi cakurya ca mainsha. Ája kwangu omi, ainkola njala tena. Munu anikubali, ainkola nyotwa tena.³⁶ Fala omi nukwambirani kuwa muniwona, novyosivyo amukubali.³⁷ Piya wanigabizire Baba wakuja kunifulata, na ája kwangu onse, simwefya panja.³⁸ Kamana nisuka kulawa binguni sijire kutenda vyanisaka omi mwanyewe ila vyasaka anipereké omi.³⁹ Vyaasaka ire anipereké omi ndi javi: kuwa piya waanipere iye, wasipoteye anta mmoja, suku ya mwinsho niwafufure.⁴⁰ Kamana vyaasaka Baba wangu ndi kuwa ammóna Mwana, akinkubali iye, akuwa na mainsha a milele. Suku ya mwinsho nomi ninfulula awe hai kwa milele.”

⁴¹ Ndimana Mayahudi wamojawapo† wakanza kunduguda konta kásema javi: “Omi ndi nkate wisuke binguni.”⁴² Ewo wakamba: “Eyu sinoyu Insa, mwana wa Yusufu, wawaye na mamaye nikamba timwijija? Sambi akwamba, ‘Nisuka kulawa binguni’, namunani?”⁴³ Insa akiwajibu: “Asani kuduguda watupu!

⁴⁴ Aapo munu ája kwangu omi bila kuvutiwa na Baba anipereké omi. Noyo munu- yo ninfulula suku ya mwinsho.⁴⁵ Nabii mmoja‡ kândika javi: ‘Piya wakuja kufundiwa na Mwenyezimungu.’ Ndi kweli kuwa piya wenye kunsikiriza Baba na warifunda kwake, wakuja kwangu omi.⁴⁶ Kusema kweli, aapo munu ammonire Baba sairí ire alawire ka Mwenyezimungu, ndi ammonire Baba.⁴⁷ Omi nukwambirani kweli kuwa mwenyé kwamini kanawo

* 6:31 Ona Zaburi 78:24, 105:40. † 6:41 “Mayahudi wamojawapo” mana ake epa ndi ware wabishána na Insa.

‡ 6:45 Ona Izaya 54:13.

mainsha a milele. ⁴⁸ Omi ndi nkate wa mainsha. ⁴⁹ Wababu zenu wârya manâ nlanga, wafwa nfululu. ⁵⁰ Eyi ndi mikate isuke mbinguni ipate munu asaka kuwa onse akirya, asifwe. ⁵¹ Nomi-nomini ndi mikate ya mainsha isuke mbinguni. Munu mmojawapo akirya noyi mikate-ysi, ainshi milele. Mikate yanukupani wanu wa mulumwengu kuwa mupate mainsha ndi mwiri wangu-wu.”

⁵² Ndimana Mayahudi wakanza kukaidiyana watupu, wakamba: “Eyu munu-yu vyataipa mwiri wake tikirya, namunani?” ⁵³ Kwa javyo, Insa akiwambira: “Omi nukwambiraní kweli: ikiwa amurire mwiri wa Binadamu wa Binguni wala amunywere damu yake[§], amuwa na mainsha nkati yenu. ⁵⁴ Mwenyé kurya mwiri wangu na kunywa damu yangu kanawo mainsha a milele, omi ninfulula suku ya mwinsho. ⁵⁵ Kamana mwiri wangu ndi mikate yakweli, damu yangu ndi kinywaji cakweli. ⁵⁶ Mwenyé kurya mwiri wangu na kunywa damu yangu, iye alungana nami, nnomi nilungana naye. ⁵⁷ Kamba Baba vyáári hai anipereké omi, nomi niwa hai kwa ajili ya Baba, ndi novyo anírya omi,akuwa na uhai julu yangu omi. ⁵⁸ Sambi, eyi ndi mikate isuke mbinguni. Siyo kamba mikate yawarire wababu zenu ikisa wakifwa. Ila ire árya eyi mikate-ysi onse akuwa na mainsha a milele.”

⁵⁹ Vinu-vi ndi vyasaowere paakiwafunda wanu nsinagoga* ya Kafarnaumu.

Wanafunzi wajibu usemi wa Insa

⁶⁰ Wanafunzi wake wengi, pawasikire usemi ure, wakamba: “Kusikira ewu usemi-wu urigariga. Epa, asikíre vyam-bire-vi, nani?” ⁶¹ Insa kejiwa mwanyewe kuwa wanafunzi wake wankuduguda kuhusu vyasaowere vire, ndimana akiwambira javi: “Usemi wangu-wu ukutipusani? ⁶² Ndimana, futi ikiwa mummona Binadamu akikwera kuludira kaákiwa mida? ⁶³ Ampa munu mainsha ndi Roho, mwiri aufái kinu. Usemi wanukwambirení umwe ndi roho na ndi mainsha. ⁶⁴ Fala katí yenu wawapo wamojawapo sawakubali.” (Insa kasowera javyo kamana kawejija tangu mida sawakubali, na kamwijijiwa

nani ája kunzungunka kumpereká ka maaduwi.) ⁶⁵ Iye akizidi kuwambira akamba: “Ndimana, nukwambiraní kuwa aapo munu ája kwangu omi iye saamuriwe na Baba.” ⁶⁶ Kwa sababu ya kusowera javyo, wanafunzi wake wengi wakilidira nyuma, awanfulate iye tena. ⁶⁷ Ndimana Insa akiwadairi mawalii kumi na wawiri ware: “Nomwe novyo, musaka muke vyenu?” ⁶⁸ Ansumani Peduru akinjibu: “Mwenye, tikuksi ka nani? Uwe ndi úri nawo masemo wakuwapa wanu mainsha a milele. ⁶⁹ Ofwe sambi tukwamini, tikwiwi kuwa uwe ndi Ntakatifu wa Mwenyezimungu.” ⁷⁰ Insa akiwajibu: “Umwe kumi na wawiri-mwe, nikamba omi ndi nukutondorení? Fala katí yenu alawirira mmoja akuwa shetwaní!” ⁷¹ Iye akimwamba Yuda, mwana wa Ansumani Shikariyoti. Kamana Yuda, ingawa ákiwa munkonjo wa ware kumi na wawiri ware, fala kanzungunka.

7

Insa paSherehe ya Vitala

¹ Bandi ya vire, Insa akenenda Galileya. Asasikire tena kwenenda makaya a Yudeya korita wakulungwa wa Mayahudi wakin-sakula wamulaye. ² Ífika karibu suku ya jambo ra Mayahudi rakwitiwa Sherehe ya Vitala. ³ Ndimana wanduze Insa ware wamwambira: “Lawa-pa, uka Yudeya, ipate wanafunzi wako newo novyo wakawone maaжуza a utendanga-yo. ⁴ Kamana munu akisaka kwijiwikana, aajuzi kufisa vitendo vyake vyatenda. Ukitenda vinu-vi, rolete baina.” ⁵ Wasema javi konta wanduze Insa awakinkubali. ⁶ Insa akiwambira: “Wakati wangu aunafika, ila wakati wenu umwe-po daima uwa tayari. ⁷ Wanu wa mulumwengu-mu umwe awakwinani, ila omi wanina, kwa sababu nilavya ushahidi kuwa vitendo vyawo vyâ ubaya. ⁸ Umwe kwerani muke kusherehe. Omi suka kusherehe-ko konta wakati wangu aunafika nfú-lulu.” ⁹ Nakuwambira javire, iye akibaki Galileya nokure.

¹⁰ Bandi ya wanduze ware kukwera kuka kusherehe kure, neye novyo akikwera akuka. Ila okire baina, kóka kwa kuri-fisafisa. ¹¹ Ndimana Mayahudi wakinsakula pasherehe pare, wakamba: “Ari, iye

[§] 6:53 Mana ake: ikiwa amumpokerere Insa na kazi yake. Mayahudi.

* 6:59 “Sinagoga” mana ake ndi nyumba ya duwa ya

noyo kawa ndepi?”¹² Noparepare wanu wengi wateta kuhusu Insa. Wengine wakamba: “Iye munu mwema” fala wengine wakamba: “Syo munu mwema, kankuwatesa wanu.”¹³ Fala awerepo munu wakusowera baina kuhusu iye konta wakiwopa wakulungwa wa Mayahudi.

Kufunda ka Insa kulawa ka Mwenyezimungu

¹⁴ Kati-kati ya suku za sherehe ire, Insa akikwera kuNyumba Takatifu, akanza kuwafunda wanu.¹⁵ Kwa javyo, Mayahudi wakitajabu wakamba: “Eyu mwananlume-yu kwijiwa evi vinu-vi piya saafundiwe namunani?”¹⁶ Insa akiwajibu, akamba: “Kufunda kanifunda siko kwangu omi, ila ndi kufunda ka ire aniperekere omi.”¹⁷ Munu mmojawapo akisaka atende vyaasaka Mwenyezimungu, basi akwijiwa kuwa eku kufunda-ku ka Mwenyezimungu au nankusowera kwa mamulaka angu mwanyewe.¹⁸ Asowéra kwa mamulaka ake mwanyewe asakula kurisifu mwanyewe. Fala ire asakúla kuwa wanu wansifu amperekere iye onse, akupo kukosa kweli kwake, iye ndi mwenyé ukweli.

¹⁹ Musa kakupani Taureti yakufulata, sinoyyo? Fala piya-mwe aapo aténda vyaasaka Taureti. Musakula kunulaya sababuni?”²⁰ Junudi ya wanu ire ikijib: “Uwe kuwa na shetwani! Asakula kukuulaya nani?”²¹ Insa akiwajibu, akamba: “Omi nitenda maajuza mamaja na piya-mwe mushanga vyanitendire.”²² Novyo-sivyo, Musa kakupani tabiya ya itani. (Kusema kweli, eyi tabiya-yi sianzire, wanza wababu zenu.) Umwe mwana nlume muntaya itani anta iwe suku ya sabadu.*²³ Onani, dalili ndi suku ya sabadu mwananlume yaataiwa itani isifufike shuruti ya Musa. Ndimana, munikimwira kwa kumponesa munu mwiri nifululu suku ya sabadu sababuni?²⁴ Musilamure kwa kunang'anizana kumaso, ila lamulani kwa shariya.”

Wanu wakaidiyana kuwa Insa Almasihi

²⁵ Kwa javyo, wanu wamojawapo wa Yerusalem wakamba: “Mwananlume wawári kunsakula kumulaya-yu, sinoyu-yu?”²⁶ Mmoneni, iye kankusowera baina wala awamwambira kinu! Itakuwa

wakulungwa wamwijiwa ka ukweli kuwa iye Almasihi?²⁷ Fala ofwe eyu tikwijiwa kwavo. Paasaka kuja Almasihi, aapo ája kumwijiwa kwavo!”²⁸ Kwa javyo Insa, paakiwafunda wanu nNyumba Takatifu, kasowera na shauti ulu, akamba: “Umwemunijiwa? Anta kwetu mukwijiwa? Fala omi sijire epa kwa kusaka omi mwanyewe. Ila aniperekere omi ndi mwenyé ukweli, iye umwe amumwijiwa.”²⁹ Fala omi nimwijiwa konta nilawa upande wake, iye ndi aniperekere.”³⁰ Basi ewo wayererakunfunga, fala aapo ankorire nkono, konta wakati wake úkiwa saunaifika.³¹ Novyo-sivyo, wanu wengi ware wankubali, wakamba: “Akija Almasihi, atakutenda alama ulu-ulu zakupunda zaatenda eyu mwananlume-yu?”

Insa akwamba kuwa akuka vyake

³² Mafarizeu wawasikira wanu wakiteta nowu mwaha-wu kuhusu Insa. Ndimana, ewo pamoja na wakulungwa wa dini wawapereka minduna wakanfunge.

³³ Noparepare Insa akamba: “Nanawo suku aba futi namwe, ikisa nukuka ka ire aniperekere.”³⁴ Mukuja kunisakula fala amuja kunipata. Mahala kanisaka kuwa omi, umwe amukidiri kuja.”³⁵ Wakulungwa wa Mayahudi wakanza kudairiyana watupu: “Noyu mwananlume-yu, ndepi kaasaka kuka ofwe tikisokerera kummona? Apurda makaya etu akuka inti za Sawari-Mayahudi, akawafunde wanu Sawari-Mayahudi?

³⁶ Paasowera, ‘Mukuja kunisakula fala amuja kunipata’, mana ake kinani? Na ‘Mahala kaniri omi, umwe amukidiri kuja’, manani?”

Insa awapa wanu maji a mainsha

³⁷ Suku ya mwinsho ya sherehe, suku iwere ulu, Insa kémira, akisowera na shauti ulu-ulu, akamba: “Ikiwa kawapo wakunkóla nyotwa, aje kwangu omi, anywe.”³⁸ Mwenyé kunikubali omi, kamba vyaasema Mandiko Matakatifu, ‘Nroho yake ibubuka miviriro ya maji a mainsha.’³⁹ Iye akamba javi kuhusu Roho wa Mwenyezimungu, kwa ware wenye kunkubali iye waja kumpokerera. Kamana nowo wakati-wo, Roho Takatifu ákiwa saanamba kuwesukira, konta Insa ákiwa saanamba kutukuziwa.

* 7:22 Shariya isema kuwa kisimana ajuzi engiziwe itani suku ya nane bandi yakupongoriwa.

Wanu wawanyika kwa sababu ya usemi wa Insa

⁴⁰ Wanu wengine pajunudi ya wanu pare, pawasikire ewu usemi-wu, wakamba: “Kweli-kwelini, eyu mwananlume-yu ndi nabii watikinrindira!” ⁴¹ Wengine wakamba: “Eyu ndi Almasihi.” Fala wengine wadairi: “Almasihi atakulawirira Galileya? ⁴² Mandiko Matakatifu[†] akwamba kuwa Almasihi ujukulu wa Daudi, sinovo? Akwamba kuwa akuja kupongoriwa inti Betlehemu kwaho Daudi, sikheli?” ⁴³ Kwa javyo, kukilawirira kwawanyikana wanu ware kwa sababu ya Insa. ⁴⁴ Noparepare wengine wakisakula wanfunge, fala aawerepo wakolosa nkono wake kunkola.

⁴⁵ Ikisa minduna waludira ka wakulungwa wa dini pamoja na Mafarizeu. Wakulungwa wawadairi minduna ware: “Umwe amujire nawo mwananlume ire sababuni?”

⁴⁶ Ware minduna ware wakamba: “Vyaasowere iye tangu anamba kusowera munu javire!” ⁴⁷ Basi, Mafarizeu ware wakiwajibu: “Mwaja? Nomwe novyo mutesiwa? ⁴⁸ Anta mmoja nkati ya wakulungwa ankubalire? Nfarizeu mmoja ankubalire?

⁴⁹ Ewu umati-wu awijiwa shariya za Musa! Ewo walaniwa!” ⁵⁰ Nfarizeu mmoja npare wakwitiwa Nikodemu, ásimanane na Insa kwa suku zipitire, iye akiwambira javi:

⁵¹ “Shariya yetu isema kuwa atijuzi kunlamula munu satinamba kunsikira ushahidi wake, tikijiwa caakosire.” ⁵² Ewo wakijibu: “Epa sambi, nowe novyo kuwa nGalileya? Unafyoma nanga kuwonerera kuwa nabii mmojawapo wakulawa Galileya aukijuzi kunrindira.” ⁵³ # [Basi wakitawanyikana, kila mmoja akuka kwake.

8

¹ Fala Insa akuka kuMwango wa Mizituni.

Mwanamuka mmoja afungiwa kwa sababu ya uzinzi

² Alufajiri, Insa akiludira nNyumba Takatifu. Wanu piya wákija naye, iye akitaka nawo, akikola kuwafunda. ³ Wanlimu wa shariya pamoja na Mafarizeu waja nawo mwanamuka ásinganiwe akizinga. Nakufika, wakimwimisa mbere ya wanu,

⁴ wakindairi Insa: “Mwanlimu, eyu mwana-muka-yu kakoriwa akizinga. ⁵ Kwa shariya yetu ofwe, Musa kâtamuru wanu kamba ewa tiapanje na mawe. Sambi uwe, ukwamba mwaja?” ⁶ Wakindairi javi wamyerere ipate wammonerere ukosa mmojawapo. Insa akinama, akanza kuremba pansi na cala. ⁷ Ikisa, kwa kuwa wakizidi kundairi-dairi, iye akitamuka, akiwambira: “Pamuri-pa, munu saanakola dambi tangu, noyo anze kulokota riwe ampanje.” ⁸ Mara tena akinama, akitidi kuremba pansi pare. ⁹ Fala ware pawasikire javire, wakilawa mmoja-mmoja, ino-ino-ino-bila nccoro. Wanzire kulawa ndi wazee. Insa wakimwasa nopare, na mwanamuka ire emire novire mbere yake. ¹⁰ Iye akitamuka, akindairi: “Nunu, ewo wandepi? Aabakire-pa anta mmoja wakusaka kuku-laumu?” ¹¹ Akinjibu: “Mwenye, aapo-pa munu anta mmoja.” Na Insa akimwambira: “Nomi novyo sukulamula hukumu. Uka vyako, usikore dambi tena.”]

Mamulaka apewe Insa na Mwenyezimungu

¹² Sambi, Insa akikola kusowera mara nyengine tena na wanu, akiwambira: “Omi ndi nuru ya mulumwengu-mu. Mwenyé kunifulata omi aashubutu kwenenda nkisi, ila apata nuru yakumpa mainsha.”

¹³ Kwa javyo, Mafarizeu wakimwambira: “Epa sambi, uwe kwankulavya ushahidi wako uwe mwanyewe, fala ushahidi wako-wo siwo bora wakutumainiwa!”

¹⁴ Insa akiwajibu, akamba: “Ingawa nilavya ushahidi wangu omi mwanyewe, fala ushahidi wangu wakweli. Kamana mahala kanilawire na mahala kanuka nukwijiwa.

¹⁵ Umwe mulamula namuna ya kibinadamu. Omi sinlamula munu. ¹⁶ Anta panilamula, kulamula kwangu ka shariya kamana omi silamula yeku yangu, nilamula pamoja na Baba aniperekere omi. ¹⁷ Anta nkati ya shariya yenu* yandikiwa kuwa, ikiwa mashahidi wawiri wasema kinu kimoja noyo, cawamba-co cakweli. ¹⁸ Omi nilavya ushahidi wangu omi mwanyewe. Baba aniperekere-yo alavya novyo ushahidi wangu omi.” ¹⁹ Kwa javyo, wakindairi: “Wawayo uwe kawa ndepi?”

[†] 7:42 Ona Mika 5:2. [#] 7:53 Mandiko a mida azipo ezi aya-zi 7:53 mpaka 8:11. ^{*} 8:17 “Shariya yenu” ndi Taureti.

Insa akijibu: "Umwe amunijiwa omi caniri na amumwijiwa Baba wangu. Munanijiwa, nanga mumwijiwa novyo Baba wangu."²⁰ Insa kasowera evi piya-vi ári nNyumba Takatifu akifunda. Iye ákiwa pansana paikikalanga kashoti ya swadaka ya Mwenyezimungu. Fala aapo anfungire, konta úkiwa saunafiga wakati wake.

Insa ndi Mwenye alawire mbinguni

²¹ Kwa mara nyengine tena, Insa akiwambira: "Omi nukuka vyangu, umwe mukuja kunisakula, fala mukufwa na dambi zenu[†]. Umwe amufika kanuka omi."

²² Ndimana Mayahudi wakambirana: "Iye akwamba kuwa ofwe atifika kooka iye-po. Iye vyamba-vi asaka kurulaya?"²³ Insa akiwambira, akamba: "Umwe mulawa pansi-pa fala omi nilawa julu mbinguni. Umwe muwa wanu wa mulumwengu nomu, omi siri wa mulumwengu-mu."²⁴ Omi nukukwambirani kuwa mukufwa na dambi zenu, konta ikiwa amukubali kuwa omi ndi noyo-noyon[‡], mukuja kufwa na dambi zenu."²⁵ Kwa javyo, ewo wakinjibu: "Uwe kuwa nani?"

Insa akiwajibu: "Omi ndi noyo wanukwambireni tangu mwanzo."²⁶ Viwapo vinu vingi vyawenye vyaniári nawo vyakukuhusuni umwe kukwambirani, na kukulamulani. Fala anipéreke omi ndi mwenyé ukweli. Vyaninsikire iye ndi vyanukwambirani mulumwengu-mu."

²⁷ Ewo awereriwe kuwa Insa akisowera kuhusu Baba.²⁸ Kwa javyo, Insa akiwambira: "Umwe pamusaka kumwimisa pamsalaba Binadamu wa Binguni, basi ndi pamusaka kwijiwa omi caniri. Mukwijiwa kuwa omi Binadamu, na sitenda kinu kwa mamulaka yangu, ila nisowera vyani-fundire Baba tu basi."²⁹ Anipéreke-yo kawa pamoja nomi. Iye aanasire yeka, kamana omi daima nitendanga vyakumwajibu iye."

³⁰ Wanu wengi pawansikire Insa akisowera javyo, wakinkubali.

Mwana wa Iburahima na mwana wa Ibilisi

³¹ Kwa javyo, Insa akiwambira Mayahudi wankubalire ware: "Umwe, ikiwa mutenda vyanukwambireni, kweli-kwelini mukuba wanafunzi wangu."³² Umwe mukuja kwijiwa ukweli, na ukweli-wo nowo

[†] 8:21 Mana ake: amuswamiiwe kwa kutowa kutubiya. niwa." Ona Kulawa 3:14.

umwe ukunusuruni."³³ Ewo wakinjibu: "Ofwe tiwa ujukulu wa Iburahima, tangu atinamba kuwa watwana wa munu. Kutisowerera kuwa tisakula kunusuriwa sababuni?"³⁴ Insa akiwajibu: "Nukwambirani kweli kuwa piya wenye kukola dambi wakuwa watwana wa dambi noyo.

³⁵ Ntwana aana pake kwa milele, fala mwana wa pakaya kanawo pake kwa milele.

³⁶ Ndimana ikiwa Mwana akukunusuruni, kweli-kwelini munusurika.³⁷ Omi nukwi-jiwa kuwa muwa ujukulu wa Iburahima. Novyo-sivyo, musaka munulaye, konta usemi wangu amutula mmyoyo mwenu.

³⁸ Omi nisowera vyanimmonire Baba wangu, umwe mutenda vyamunsikire wawa yenu."³⁹ Ewo wakinjibu, wakamba: "Ofwe wawa yetu Iburahima."

Insa akiwambira: "Umwe, munawa wana wa Iburahima, nanga mufulata vyaákitendanga Iburahima."⁴⁰ Fala umwe musaka munulaye, omi níri kukwambirani ukweli waninsikire Mwenyezimungu. Iburahima atendire javyo.⁴¹ Umwe mwankutenda vitendo vya wawa yenu."

Ewo wakimwambira: "Ofwe atiri wana wa zinaa, tanawo wawa mmoja tu basi, Mwenyezimungu!"⁴² Insa akiwambira: "Inawa Mwenyezimungu Baba wenu, umwe nanga munipenda omi, konta omi nilawa ka Mwenyezimungu, niwa epa. Sirjisire omi mwanyewe, ila iye ndi anipereke.

⁴³ Umwe amwereriwa vyanukwambirani-vi, sababuni? Ndi kwa kuwa avikwajibuni kufulata usemi wangu.⁴⁴ Umwe wawa yenu ndi Ibilisi, na umwe vikwajibuni kutenda vimwajibu wawa yenu. Iye tangu mwanzo kisomi, enendera njira ya ukweli, konta ukweli wawenye aana. Ibilisi paalongopa, atenda vitendo vya tabiya yake, kamana iye nlongo, ndi wawa wa walongo.⁴⁵ Fala omi, kwa kuwa nukwambirani kweli, umwe amunikubali.

⁴⁶ Pamuri-po, nani akidiri kwakikisha kuwa nanawo dambi? Ikiwa nankukwambirani ukweli, umwe amunikubali sababuni?⁴⁷ Ari ka Mwenyezimungu onse, asikiriza caasema Mwenyezimungu. Sababu umwe amusikiriza ndi kwa kuwa ámuri ka Mwenyezimungu."

Insa ndi mwenyé kuwepo tangu mwanzo

[‡] 8:24 Epa Insa katumira zina ra Mwenyezimungu, "Omi

⁴⁸ Mayahudi wakinjibu, wakamba: “Atina haki yakukwambira kuwa uwe kuwa nSamariya, na kwanawo shetwani?” ⁴⁹ Insa akijibu: “Omi sina shetwani ila ninsifu Baba wangu, umwe amunisifu. ⁵⁰ Wala omi sisakula kuritkuza omi mwanyewe. Kawapo mwengine asakula kutukuziwa kwangu omi, iye ndi mwenyé kulámula.

⁵¹ Omi nukwambirani kweli: munu akifulata usemi wangu, kwa milele aayeza kifo.”

⁵² Mayahudi wakimwambira javi: “Sambi tikijiwa kuwa uwe kwanawo shetwani! Iburahima kafwa na minabii wafwa, fala uwe ukwamba, ‘Munu akifulata usemi wangu, kwa milele aayeza kifo.’” ⁵³ Uwe auri bora wakunzaidi baba wetu Iburahima afwire? Minabii novyo wafwa. Sambi uwe uritula kuwa nani?” ⁵⁴ Insa akijibu: “Ikiwa omi niritikuza mwanyewe, utukufu wangu aufai kinu. Anitíkuza omi ndi Baba, noyo wamwámba kuwa ndi Mwenyezimungu wenu-yo. ⁵⁵ Fala umwe iye amumwijiwa, ila omi nimwijija. Omi nikamba simwijiwa, nukuwa nlongo kamba umwe. Falakini omi kweli-kwelini nimwijija, na usemi wake nifulata. ⁵⁶ Baba wenu Iburahima kafurahi konta kejiwa kuwa nukuja. Iye kawona na kawa radi.” ⁵⁷ Kwa kusema javyo, Mayahudi ware wakimwambira javi: “Uwe aunatimu myaka amusini. Iburahima-yo kúmmona?”

⁵⁸ Insa akiwajibu: “Omi nukwambirani kweli: kábula yakupongoriwa Iburahima, omi niwapo.” ⁵⁹ Basi wakilokota mawe kusaka kumpanja, fala Insa akirifisa, akilawa nNyumba Takatifu mure.

9

Alama yasita yolete vyáári Insa: amponesa munu sawona

¹ Insa paakipita, kammona munu sawona tangu kupongoriwa kwake. ² Wanafunzi wake wakindairi: “Mwanlimu, mwananlume-yu kapongoriwa sawona kwa sababu ya dambi zake au za wawaze?” ³ Insa akiwajibu: “Eyu kutowa kuwona kuno siyo kwa sababu ya dambi zake wala za wawaze, ila ipate julu yake viwoneke vyataenda Mwenyezimungu. ⁴ Ofwe tijuza tikore kazi za ire anitumire nsana nowu. Ukuja usiku sauqidirika kukoriwa kazi. ⁵ Paniri-pomulumwengu-pa, omi ndi nuru ya mulumwengu-mu.” ⁶ Nakwisa kusema javire,

* 9:6 Kigeregu: “akintawaza”.

akisunira pansi, akivulula nsanga ure na mata, akimpaka* mwananlume ire mmaso, ⁷ akimwambira javi: “Uka, ukataye kumaso tanki ulu ya Siloamu.” (Zina ra Siloamu mana ake “kaperekiwa”.) Basi, mwananlume ire akuka, akitaya kumaso, akiludira ukaya wakuwona wawenye ngwee.

⁸ Kwa javyo, majirani wake wákimonanga vyáákiwa, pamoja na wanu wákimonanga akipita akilebelia zimola, wakamba: “Eyu sinoyu-yu mwananlume ákikalanga akilebelia zimola-yu?” ⁹ Wanu wengine wakamba: “Aye, ndi noyu.” Fala wengine wakamba: “Siye! Eyu kalandana naye tu basi.” Iye akizidi kwamba: “Ndi nomi.” ¹⁰ Kwa javyo, ewo wakindairi: “Sambi, maso ako-yo afunguka mwaja? Uwonaja?” ¹¹ Iye akijibu: “Mwananlume wakwitiwa Insa ndi avulure nsanga na mata akinipaka mmaso-mu, akinambira javi: ‘Uka ukataye kumaso Siloamu.’ Nomi nukuka, nikowa, nikanza kuwona!” ¹² Ewo wakindairi: “Noyo mwananlume-yo kawa ndepi?”

Iye akijibu: “Sijiwa.”

¹³ Ikisa ewo wakintwala mwananlume saákiwona ire, wakuka naye ka Mafarizeu.

¹⁴ Kusema kweli, suku Insa yaávulure nsanga na mata, akimponesa mwananlume saakiwona ire, íkiwa suku ya sabadu.

¹⁵ Kwa javyo, Mafarizeu ware newo novyo wakindairi tena namuna vyaponesiwe awone. Iye akiwambira: “Iye kavulula nsanga na mata, akinipaka mmaso-mu, ikisa nikitya kumaso, nikanza kuwona ngwee.”

¹⁶ Mafarizeu wamojawapo wakamba: “Eyu munu-yu aaperekwiwe na Mwenyezimungu, kamana aafulata shariya ya sabadu.” Fala wengine wadairi: “Munu mmadambu atendaja maajuza kamba-ya?” Noparepare wakawanyana.

¹⁷ Ndimana Mafarizeu ware wakindairi saakiwona ire mara nyengine tena: “Kwa kuwa kakufungula maso ako, kuhusu iye waambani?”

Iye akijibu: “Iye nabii.”

¹⁸ Wakulungwa wa Mayahudi ware awakinkubali kuwa aakiwona tangu kupongoriwa kwake, akiludira kuwona, mpaka wakiwetisa wawaze mwananlume aponesiwe ire. ¹⁹ Nakufika wawaze, ewo

wakiwadairi: "Eyu mwanenu wamwamba kapongoriwa sawona-yu? Epa sambi kanza kuwona mwaja?"²⁰ Wawaze ware wakijibu, wakamba: "Tikwijiwa kuwa eyu mwanetu, na kâpongoriwa sawona."²¹ Fala vyenende akanza kuwona atijiwa, wala atimwijiwa munu mmojawapo amponese. Iye munu nzima wawenye, ndairini mwanyewe, akisaka akujibuni!"²² (Wawaze ware wasowera javire kwa sababu yakuwopa wakulungwa wa Mayahudi, kamana wakulungwa ware wâsikizana kuwa wantuwise ndaraja ya nsinagoga munu mmojawapo asâka kuwambira wenzive kuwa Insa Almasihi.)²³ Ndimana wawaze ware wajibu javi: "Iye munu nzima, ndairini mwanyewe!"

²⁴ Kwa javyo, mara yapiri ewo wakimwita mwananlume saakiwona ire, wakimwambira: "Kwa kutukuziwa Mwenyezimungu, sema kweli yako! Ofwe tikwijiwa kuwa eyo munu-yo mmadambi."

²⁵ Akijibu: "Kamba iye mmadambi omi sijiwa. Canijiwe omi kinu kimoja: ingawa sîkiwona, fala sambi nankuwona!"²⁶ Ewo wakindairi: "Iye kakutenda kinani? Kakuponesa mwaja?"²⁷ Iye akiwajibu: "Omi nûkwambirani futi, fala umwe amusikire. Musaka kusikira tena sababuni? Nomwe novyo musaka muwe wanafunzi wake?"²⁸

Ewo wakintukana cwaa, wakamba: "Epa, uwe kuwa mwanafunzi wake, fala ofwe tiwa wanafunzi wa Musa!"²⁹ Ofwe catijiwe ndi kuwa Mwenyezimungu kasowera julu ya Musa, fala kuhusu eyu, atimwijiwa anta upande waalawirire!"³⁰ Mwananlume ire akiwajibu, akamba: "Mama! Mbana vishangisa! Umwe amwijiwa kalawirira, fala iye omi kaniponesa."³¹ Tikwijiwa kuwa Mwenyezimungu aawasikiriza wamâdambi, fala awasikiriza wenye kumwishimu, watimiza vyasaaka iye.

³² Tangu mwanzo wa ulumwengu, hapana manziro kasikirkana kuwa munu mmojawapo kamponesa munu waâkupongoriwa sawona.³³ Inawa eyu munu-yu aajire kulla ka Mwenyezimungu, aangari kutenda kinu kamba-ci."³⁴ Ewo wakinjibu: "Uwe kuwa mmadambi nfululu! Sambi, uyerera kutifunda ofwe mwaja?" Noparepare wakintuwisa wakinlavira panja ya sinagoga

[†] 9:38 Atina uhakika aya 38 na 39 kuwa ziwapo mmandiko matanzi. ^{*} 10:9 Kigeregu: "Akwingira, alawa, na apata cakurya."

ire.

³⁵ Insa paasikire kuwa wantuwisira panja, akinsingana mwananlume ire, akindairi: "Uwe, unkubali Binadamu wa Binguni?"³⁶ Mwananlume ire akijibu, akamba: "Noyo nani, Mwenye? Nambire, ipate ninkubali!"³⁷ Insa akimwambira: "Uwe kummona, ndi noyu-noyuni wauri kusowera naye sambi-pa-yu!"³⁸ †[Iye akamba: "Mwenye, nukwaminil!" Nayé akimwabudu.³⁹ Insa akimwambira:] "Omi njia mulumwengu-mu niwalamure wanu. Nija ipate vipofu wawone, na wawona wawe vipofu."⁴⁰ Mafarizeu wengine waâkiwa nawo karibu iye wansikire akisowera javire, wakindairi: "Epa, ikuwa ofwe novyo tiwa vipofu, nikamba?"⁴¹ Insa akiwajibu: "Inawa umwe muwa vipofu, amungari kuwa na wamâdambi! Fala kwa kuwa mukwamba 'Tiwona', salani na madambi yenu."

10

Insa ndi Nryango na Nsunga mwema

¹ Insa kazidi kusowera, akamba: "Omi nukwambirani kweli. Akwéra sereka ya makondoo onse, kwasa kupita panryango, noyo-noyonu mwivi na nnyang'anyi.

² Fala apita panryango onse, ndi nsunga wa makondoo. ³ Kwake iye nakola wa panryango wa sereka ndi afungúla nryango. Makondoo wamanyira shauti yake. Aweta makondoo mazina awo, newo awasungira panja. ⁴ Bandi yakuwalavira piya panja, iye alongorera. Makondoo wanfulata konta wamanyira shauti yake.

⁵ Munu sawamwijiwa awanfulata ila wantira, konta awamanyira shauti za wanu sawawejiwa."⁶ Insa wanu ware kawasowerera eci kinyume-ci, fala ewo awererewe mana ake vyawambiriwe vire.

⁷ Kwa javyo, Insa akiwambira tena: "Nukwambirani kweli. Omi ndi nryango ka makondoo. ⁸ Piya walongorere kâbula ya omi wevi na wanyang'anyi, na makondoo awasikirize. ⁹ Omi ndi nryango. Anipita akingira julu yangu omi onse, avushiwa. Kanawo mahala pakutumaini.* ¹⁰ Mwivi

* 10:9 Kigeregu: "Akwingira, alawa, na apata

aaja sairi kuja kwiwa, kuulaya na kudan-gula. Omi ni ja ipate wawe na mainsha, wawe nawo pakulu pawenye.”

¹¹ Insa akizidi kusowera, akamba: “Omi niwa Nsunga mwema. Nsunga mwema apereka mainsha ake afwe kwa ajili ya makondoo wake. ¹² Nsunga wakupokeresiwa, nsunga-yo makondoo siwakewakeni. Iye siyo nsunga wa kweli. Ndimana, akimmona mmwinzi akija, atuwa, awasa makondoo. Basi mmwinzi anduru kondoo mmoja, wengine watawanyikana. ¹³ Kwa kuwa nsunga wakupokeresiwa awashugu-likira makondoo. ¹⁴ Omi niwa Nsunga mwema. Niwejiwa makondoo wangu, newo omi wanijiwa, ¹⁵ kamba Baba vyaniyiwa, nomi nimwijiwa Baba. Omi nipereka mainsha angu nifwe kwa ajili ya makondoo wangu. ¹⁶ Nanawo makondoo wengine sawapo eci kitundu-ci, newo novyo nijuzi niwalongoze. Ewo wakuja kusikira shauti yangu. Kwa javyo, uwapo nfuwo moja na nsunga mmoja. ¹⁷ Baba anipenda kwa kuwa nipereka mainsha angu nifwe, niludire kutwala tena. ¹⁸ Hapana alávyä mainsha angu, ila omi niripereka mwanyewe nifwe. Nanawo mamulaka a kupereka, na nanawo mamulaka a kupewa kupokerera tena. Ndi vyanilaiziwa na Baba wangu.”

¹⁹ Kwa mara nyengine tena, kukilawirira kwawanyana nkati ya Mayahudi kwa sababu ya nowu usemi-wu. ²⁰ Wengi wakamba: “Iye kapatiwa na shetwani, kangami! Noyu musikiriza sababuni?”

²¹ Wengine wakamba: “Usemi-wu siwo wa munu wakumilikwa na shetwani. Shetwani amponesa munu sawona?”

Insa na Baba kinu kimoja

²² Nowo wakati-wo, Yerusalemu ritendiwa Jambo ra Nyumba Takatifu[†]. Úkiwa wakati wa baridi. ²³ Insa akipita akenenda nlupenu ra Nyumba Takatifu, lupenu-ro rikitwa “Lupenu ra Selemani”.

¹ Mida-na-midada, Mwenyezimungu kásowera na wababu zetu mara nyingi zawenye, kwa namuna nyingi zawenye, julu ya minabii. ² Fala sambi, suku za mwinsho-*zi*, kasowera nofwe julu ya Mwanawe, aturiwe na Mwenyezimungu kuwa mwenyé irati wa vinu piya, na iye ndi ire julu yake Mwenyezimungu ombire vinu piya. ³ Mwana-*yo* ndi nlangaza wa utukufu wa Mwenyezimungu, na atolotera kweli-kwelini vyaari Mwenyezimungu. Vinu piya mulumwengu-mu viwankwikala kwa uwezo wa ámuri zake. Bandi yakutimiza kazi yake yakuswafi madambí, kekala nnkonono-nriro wa Mwenye Nkulu mbinguni, ⁴ kwa kuwa kantula kuwa bora pakulu sana zaida ya malaika, kamba zina raritire rakuwa na mamulaka pakulu zaida ya mazina a malaika.

⁵ Ndi kweli konta Mwenyezimungu tangu aanamwambira laika wake mmojawapo javi*: _____

* 1:5 Ona 2 Samuweli 7:14; Zaburi 2:7. † 1:5 Ona 2 Samuweli 7:14. ‡ 1:6 Ntanzi akiwa nriti wa vinu piya vya wawaye. § 1:6 Ona Kumbukumbu 32:43. * 1:7 Ona Zaburi 104:4. † 1:8 Ona Zaburi 45:6,7. ‡ 1:10 Ona Zaburi 102:25-27.

“Uwe kuwa mwanangu, omi rero nanza kuwa wawayo.”

Na tena, aanamwambira laika mmojawapo javi†:

“Omi nukuja kuwa Baba wako na uwe ukuja kuwa mwanangu.”

⁶ Visitoshe Mwenyezimungu, paawere tayari kumpereká Mwanawe ntanzi‡ mulumwengu-mu, kaamba§:

“Piya malaika wa Mwenyezimungu wamwabudu.”

⁷ Kuhusu malaika kaamba javi*:

“Mwenyezimungu awatenda malaika wawe kamba mepo, watumisi wake wawe kamba malulimi a moto.”

⁸ Fala kuhusu Mwanawe, akwamba javi†:

“Uwe Mwenyezimungu, útawala daima milele.

Úwatawala wanu muufalume wako kwa shariya.

⁹ Kwankupenda ukamilifu na wankukukima ubaya.

Kwa javyo, omi Mwenyezimungu, Nlungu wako, nukumimiranira mafuta a radi pakulu koliko wenziwo piya.”

¹⁰ Mwenyezimungu kamwambira Mwanawe tena‡:

“Mwenye, tangu mwanzo, uwe ndi uturire aluserusu ya duniya, na kwa makono ako kumba bingu piya.

¹¹ Evyo piya-vyo vílainika, fala uwe kuwapo daima.

Avija kufái kinu, kamba nguwo zaku-papuka.

¹² Kamba Zubáu ya mida, ndi vyauja kukunja, kamba munu vyaaluriza nguwo, uwapindula.

Fala uwe ndi nowe wa daima,

* 1:5 Ona 2 Samuweli 7:14; Zaburi 2:7. † 1:5 Ona 2 Samuweli 7:14. ‡ 1:6 Ntanzi akiwa nriti wa vinu piya vya wawaye. § 1:6 Ona Kumbukumbu 32:43. * 1:7 Ona Zaburi 104:4. † 1:8 Ona Zaburi 45:6,7. ‡ 1:10 Ona Zaburi 102:25-27.

kuinshi kwako akuna mwinsho.”

¹³ Mwenyezimungu laikani wamwambire suku moja javi[§]:

“Ikala mahala bora-pa upande wangu wa nkono nriro-wu,
mpaka maaduwi wako niwature kumaulu kwako?”

Malaika-wo wa kinani? ¹⁴ Piya-wo siroho zintumika Mwenyezimungu na awaperekwiwe kuwasaidiya wanu waja kuvushiwa?

2

Nafasi ulu yakuvushiwa

¹ Ndimana, tijuzi titengemane tifulate pakulu vyatisikira ipate tisipoteye.

² Kamana habari zereziwe na malaika zoloka, watúpa shariya onse na wabishi wapata hukumu iwajúzire ³Kwa javyo, futi ofwe ikiwa atiyeriwa tisaka kunusurikaja na kuvushiwa kukulu-ko? Kuvushiwa-ko ndi kwanzire kwereziwa na Mwenye mwanyewe, ikisa wasikire watakikisha kuwa kwei. ⁴Mwenyezimungu neye novyo ázidi kwakikisha kuwa habari-zo zakweli julu ya alama, matajabisa, maajuza a uwezo jisijisi, na julu yakutisira uwezo wa Roho Takatifu, sawa-sawa na vyasaka mwanyewe.

Insa Almasihi áfungula njira tivushiwe

⁵ Mwenyezimungu aawapere malaika uwezo wakutawala ulumwengu mupya* watamba-wu. ⁶Fala mMandiko Matakatifu mamojawapo† kalavya ushahidi javi:

“Yarabi Mwenyezimungu,
binadamu nani wakummwaza?
Binadamu akuyeri kakinani?

⁷Kuntula utoto aba kawa sini ya malaika, kunkonga lemba ra utukufu na inshima,
⁸kutula piya sini ya kumaulu kwake.”

Sambi, payambiwa kuwa “kutula piya sini yake”,
mana ake ndi kuwa acipo anta kimoja saciri sini yake.

§ 1:13 Ona Zaburi 110:1. * 2:5 Ulumwengu mupya ndi namuna nyengine zawaja kuinshi wenye kuvushiwa na Insa.

† 2:6 Zaburi 8:4-6. † 2:12 Ona Zaburi 22:22. § 2:13 Ona Izaya 8:17. * 2:14 Kigeregu: “wanawo nyama na damu”.

Fala sambi-pa wanu atiri kuwawona piya sini yake.

⁹ Ila tankummona iye kuwa, kwa wakati aba, káturiwa utoto koliko malaika. Iye Insa ndi ayerere kifo, julu ya rehemaya Mwenyezimungu, kwa ajili ya wanu piya. Ingawa káturiwa utoto, fala sambi-pa, kwa sababu ya kutabika ka kifo, iye kakongiwa lemba ra utukufu na swifa!

¹⁰Kamana iwapo shariya kuwa Mwenyezimungu, mwenyé vinu piya na mwenyé kumba piya, aje nawo wafulati wengi wawe upande wa utukufu wake. Katenda javyo julu ya kuntenza Insa, awalóngiza wanu kuwavusha, awe kamilifu julu ya kutabika.

¹¹ Kamana ire atakátfi, na ware watakatífiwa, walawirira ka Baba mmoja. Ndimana Insa aawona haya kuweta “wanduzangu”,

¹²kamba vyayambiwe mMandiko‡:

“Níwerezabaina vyautendanga uwe wanduzangu.

Nukwimba nukukusifu mbere ya wanu wako.”

¹³ Mmandiko mengine, iye kaamba javi[§]:

“Omi níntumaini Mwenyezimungu.”

Ikisa kaamba tena:

“Niwa epa, na ware Mwenyezimungu wau-naminire kuwasunga,
ewo wawa kamba wanangu.”

¹⁴ Sambi, ware wetiwe wanawe na Insa, kwa kuwa ewo binadamu*, iye mwanyewe kálawirira kwa namuna moja ipate julu ya kifo cake, anshinde ire ári na uwezo wa kifo, Ibilisi. ¹⁵Kwa namuna-yo, piya wákiwa watwana kwa milele kwa sababu ya kopa kufwa, Insa kawanusuru. ¹⁶Kamana vikwi-jiwikana kuwa aajire kuwasaidiya malaika, ila kája kusaidiya ujukulu wa Iburahima.

¹⁷Ndimana neye akijuzi awe sawa-sawa na wanduze kwa kila namuna, ipate awe nlongozi nkulu wa dini wakuwa ndi mwanyé huruma na mwaminifu. Kwa namuna-yo, antumike Mwenyezimungu, iye mwanyewe awe kafara, ipate madambi a wanu aswami-iwe. ¹⁸Kamana, kwa kuwa katabika julu

ya kushetwaniwa, iye kanawo uwezo wa kuwasaidiya ware wenyekushetwaniwa.

3

Insa ndi nkulu zaida ya Musa

¹Kwa javyo umwe, wanduzangu watakatifu, wenzangu titiwe mbinguni, akuyerini Insa. Iye ndi walii na nlongozi wetu nkulu wa dini yatiri kwereza-*yi*. ²Kamba Musa vyaákiwa mwaminifu na kazi yake nnyumba ya Mwenyezimungu*, na Insa ákiwa mwaminifu ka Mwenyezimungu mwenyé kuntondola. ³Musa kasifiwa, fala Insa kawoniwa kuwa ndi wakujúzi kusifiwa pakulu zaida ya iye, kamba njengi wa nyumba vyaasifiwa pakulu koliko nyumba yawenye. ⁴Kamana kila nyumba ítengезiwa na munu, ila atengéza vinu piya Mwenyezimungu. ⁵Musa ákiwa ntumisi mwaminifu nnyumba ya Mwenyezimungu piya, kalavya ushahidi wa vire víkija kwereziwa mbere. ⁶Fala Insa Almasihi mwaminifu kamba mwana, amiri wa nyumba-*yo*. Na nyumba-*yo* ndufwe, ikíwa tizídi koloka mpaka mwinsho, na hakika na kwamini nkati ya tamaa yatirindira.

Ukosofu wa kutowa kwamini

⁷Kwa javyo, kamba vyaamba Roho Takatifu† javi:

“Rero, mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,
⁸myoyo yenu musitaye ugumu,
 kamba wababu zenu pawâbishane nami,
 suku yawâniyerere nlanga.
⁹Emo wababu zenu wâniyerera waniwone
 canikisaka kutenda,
 ingawa wâwona vyanisaidiye muda wa
 myaka arubaini.
¹⁰Ndimana nkimiwa na noco kizazi-co,
 nikisowera javi:

‘Daima wankukosa mmyoyo mwawo,
 wakatala kufulata njira zangu.’

¹¹Kamba vyaniflapike paníkimiwe, nikamba:
 ‘Awaja kwingira mahala pangu papumuzi.’

¹²Wanduzangu, more-more asilawirire munu nkati yenu wakuwa na moyo mbaya wakutowa kwamini, wakulongoza kukatala

kunfulata Nlungu hai. ¹³Kwasa javyo, zidini kurimbisana myoyo kila suku sambi nopa pamwitiwe-pa, ipate asilawirire nkati yenu munu wakutaiwa moyo ngumu, wakuteseka na dambi. ¹⁴Kamana kwamini kwetu katiwere nawo tangu mwanzo, tikizidi koloka mpaka mwinsho, tilawirira kuwa wenziwe Almasihi nkati ya kazi yake. ¹⁵Ndi kamba vyayambie‡:

“Rero, mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,
 myoyo yenu musitaye ugumu,
 kamba wababu zenu pawâbishane nami.”

¹⁶Epa wasikire shauti ya Mwenyezimungu wakibishana naye ndi wepi? Kusema kweli, sipiya walongoziwe na Musa kulawa Miswiri? ¹⁷Na ware Mwenyezimungu waakimiyane nawo muda wa myaka arubaini ndi wepi? Siware wakorire dambi, wakifwira nlanga nomo? ¹⁸Na paalapire kuwa “awaja kwingira mahala pangu papumuzi”, waakiwamba ndi wepi? Siware watupire kauli zake? ¹⁹Basi, tereriwa kuwa awakidire kwingira kwa sababu ya kutowa kutumaini.

4

¹Kwa kuwa tanawo mpaka sambi-pa tamaa yakwingira mahala pake papumuzi, tiritunze sana-sana ipate asilawirire mmoja wenu wakusokerera kwingira nopo mahala-po. ²Kamana teréziwa Habari Ngema kamba vyawereziwe ewo*, ila ewo cawasikire aciwafaire kinu, kwa kuwatowa umoja wa kwamini cawasikire. ³Basi, ofwe wenyekwamini tingira nopo mahala papumuzi-po, kamba vyaâmbire Mwenyezimungu javi†:

“Kamba vyanilapire nkati ya nyongo yangu:
 ‘Awaja kwingira mahala pangu papumuzi.’”

Kasowera javyo ingawa kazi yake kâtimiza tangu pawsire kumbiwa ulumwengu. ⁴Kamana kuhusu suku yasaba, nsitari mmoja wa Mandiko‡ ukwamba javi:

* 3:2 “Nnyumba ya Mwenyezimungu” mana ake “nkati ya Mwenyezimungu”. † 3:7 Ona Zaburi 95:7-11. ‡ 3:15 Ona Zaburi 95:7; Waebraniya 3:7. * 4:2 “Ewo” ndi ware wákiwa nlanga. † 4:3 Ona Zaburi 95:11. ‡ 4:4 Ona Mwanzo 2:2.

“Suku yasaba Mwenyezimungu kapumula kwa kutimiza kazi zake piya.”

⁵Usowezi mmoja nowo uwiriziba tena:

“Awashubutu kwingira mahala pangu papumuizi.”

⁶ Kwa kuwa wanzire kwereziwa Habari Ngema awengire kwa kutowa kusikiriza, wengine wapewa nafasi yakwingira nopo mahala papumuizi-po. ⁷ Tukwijiwa kinu kamba-ci konta Mwenyezimungu katula suku nyengine, kaamba kuwa ndi suku ya “rero” pairipo nafasi yakwingira mahala papumuizi-po. Kwa myaka mingi ipitire, Mwenyezimungu kâsowera julu ya Daudi, kamba vyambo futi:

“Rero mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,
myoyo yenu musitaye ugumu.”

⁸ Kamana inawa Yoshwa wanu-wo kawalongoza mahala papumuizi, aikibidi Mwenyezimungu kusowera tena, kutula suku nyengine. ⁹ Kwa javyo, kamba Mwenyezimungu vyAAPUMURE suku yasaba pesire kumba ulumwengu, ingaripo nafasi ya wanu wa Mwenyezimungu kupumula. ¹⁰ Kamana mwenyé kwingira mahala papumuizi pa Mwenyezimungu ápumula kazi zake sawa-sawa vyAAPUMURE Mwenyezimungu kazi zake.

¹¹ Basi, mahala papumuizi-po, titende juhudji tingire, ipate asiwepo wakunkuna kamba vyavivakunire mida, wakutowa kwingira kwa sababu ya ubishi.

¹² Kamana usemi wa Mwenyezimungu uwa nawo uhai na nguvu, unoréka pakulu kupunda jambiya yakusinja kuno na kuno. Úpitirira mpaka mmoyo, ukwawanya moyo na roho kamba jambiya vyayawanya nyama na makongolo. Ndimana usemi wa Mwenyezimungu úkidiri kwawanya mawazo meema na mabaya a mmoyo. ¹³ Aapo kiyumbe akidiri kufisa siiri mbere ya Mwenyezimungu. Kwake iye, piya viwa paweru, awona vinu piya na maso ake. Na vitendo vyatitenda tijuzi kunjibu.

§ 4:14 “Mwana wa Mwenyezimungu” ndi zina rimojawapo retiwa Insa. Rikolota kupatana kwema ka Insa na Mwenyezimungu, kamba mwana na wawaye. Eri zina-ri aisema kuwa cipita kitendo ca muka na nilume, ila kupatana kukulu ka kiroho. * 5:5 Ona Zaburi 2:7. † 5:6 Ona Zaburi 110:4.

Insa atipendeleya mbere ya Mwenyezimungu

¹⁴ Sambi, kwa kuwa tanawo nkulungwa nkulu wa dini atangurire binguni, Insa, Mwana wa Mwenyezimungu[§], tukeni tikore makono mawiri kwamini kwetu katereze. ¹⁵ Kamana nlongozi wetu nkulu wa dini akidiri kutiwonera utungu ufuko wetu, kwa kuwa kashetwaniwa kwa namuna-zi piya kamba vyatishetwaniwa ofwe, ila iye aakorire dambi. ¹⁶ Basi, tukeni na uhakika tiwe karibu na kiti ca Mwenyezimungu, tipate huruma na rehema patisakula kusaidiiwa.

5

¹ Kila nkulu wa wakulungwa wa dini ákitondoriwa nkati ya wanu, akitawaziwa ipate antumike Mwenyezimungu kwa faida ya wanu. Kazi yake ūkiwa yakuperekwa kafara na swadaka ipate wanu wafutiwe madambi awo. ² Watikínifu na sawári makamilifu, iye ákidiri kuwanonera utungu, kwa kuwa iye mwanyewe kaveya.

³ Kwa javyo, ájuzi aperekwa kafara kwa madambi ake iye mwanyewe kamba vyaalavya kafara kwa madambi a wanu wengine. ⁴ Na hapana munu wakuritawaza mwanyewe cewo cakusifiwa-ci, ila akolotiwa na Mwenyezimungu kamba vyavíunkire Aruna.

⁵ Kwa namuna moja noyo, Almasihi aaritawaze iye mwanyewe ubora wakuwa nkulungwa wa dini. Ila Mwenyezimungu kantondola, akimwambira* :

“Uwe kuwa mwanangu,
lero omi nukupongola.”

“Na mahala pengine†, akwamba tena javi:

“Ukuwa nlongozi wa dini wa milele,
kamba vyawere Melkizideki.”

⁷ Insa, mainsha ake mulumwengu-mu, akilebelanga duwa ka Mwenyezimungu, mwenyé uwezo wakunvusha nkati ya kifo. Akilebelanga kwa shauti ulu-ulu kuno akinlawa masozi. Na akisikiriziwa kwa sababu ya kunyenyekeya kwake kutenda

vyaasaka Mwenyezimungu. ⁸ Ingawa ákiwa mwana, karifunda kutwii julu ya tabu zimpatire. ⁹ Na paatimize vinlazimire kutenda, kalawirira kuwa Nvushi wa milele wa piya wenye kunfulata. ¹⁰ Na Mwenyezimungu kantula kuwa nkulu wa wakulungwa wa dini, kwa namuna moja noyo kamba vyákiwa Melkizideki.

Usase kuntumaini Insa Almasihi

¹¹ Kuhusu ewu mwaha-wu[‡], tanawo vinu vingi vyawenye vyakukwerezani. Fala virigariga kukwerezani konta amusaka kweleriwa. ¹² Kamana, ingawa upita wakati mwingi, mujuzi muwe wanlimu, fala mun-sakula munu akufundeni vinu vyakwanza vya habari za Mwenyezimungu. Muwa kamba watoto musakula kujiji maziwa, iri hali mukijuzi murye cakurya cakumatiwa. ¹³ Kamana ajúzi kunywa maziwa onse angari toto, ndi sejiwa cema. ¹⁴ Fala cakurya cakukamatiwa ndi cankulungwa. Kwa njira ya kufundiwa, ewo wanawo ankili yakutondola cema na kibaya.

6

¹ Kwa javyo, tase vyatanzire kurifunda kuhusu Almasihi, tukeni mbere mpaka tififikire vyakurifunda vyakukamilika. Tisijenge tena upya aliserusu zakufulata ngano kamba ezi: cakwaniza, ibidi kutubiya vitendo vyakuja na kifo, na kurimbirira kuntumaini Mwenyezimungu;

² capiri, kufunda kuhusu koza, alama ya kutubiya; catatu, kuntula munu makono; caane, kuwafufula wanu ka wafwi; na catanu, kulamuriya ka milele.

³ Nevyo, Mwenyezimungu akisaka, titenda.

⁴ Kamana ware wasire kunkubali Insa, aapo akidiri kuwaludisira kutubiya tena upya. Ewo mara moja wâpokerera nuru ya Mwenyezimungu, wâyeza thawabu ya binguni, wâpokerera Roho Takatifu pamoa na wenziwaho. ⁵ Wâyerera wema wa usemi wa Mwenyezimungu, na wâyerera vitendo vya uwezo visaka kukuna paaja kutawala Mwenyezimungu. ⁶ Fala novyo-sivyo, wantula minyongo iye! Aapo akidiri kuwaludisira kutubiya tena, konta wankejeli baina

Mwana wa Mwenyezimungu, wangomezera tena mpaka warihukumu.

⁷ Kamana ewo wawa kamba ardhi inywa maji a nvula painya ponse. Ikiwa ardhi-yo iruwerya miti ya kuwafái warimi, ardhi-yo ijanliiwa na Mwenyezimungu. ⁸ Fala ikiwa ardhi-yo iruwerya miti ya miwa na mbiriwiri, saifái na karibu yakulaniwa. Ardhi-yo mwinshoni ikociwa.

⁹ Wapendani wangu, ingawa tisowera javi, titumaini kuwa umwe mwanawo vinu vyema pakulu, vyakuja na ku-vushiwa. ¹⁰ Kamana Mwenyezimungu ndi mwenyé shariyi, akwijija camutenda, na namuna vyamuwapenda wenzenu kwa zina rake, pamuwasakiya watakatifu, na mpaka sambi-pa mungari kutenda novyo. ¹¹ Vitajibu pakulu kuwa umwe-po kila mmoja olete juhudji moja mpaka mwinsho, ipate muwe na uhakika wa tamaa yamurindira na imani. ¹² Nkati ya kwamini kwenu, musiwe wafuko, ila muwafulatize ware wariti tamaa julu ya kutumaini na imani.

Mwenyezimungu atimiza tamaa yake

¹³ Mwenyezimungu, paampere tamaa Iburahima, kârilapira mwanyewe kuwa atimiza tamaa yake, konta aawerepo mwengine wakunzaidi iye. ¹⁴ Iye kaamba*:

“Nilapa ka ukweli kuwa uwe nukujanliya pakulu, nukupa ukujulu mwingi wawenye.”

¹⁵ Ndimana Iburahima, kwa kuwa akirindira na imani, tamaa ire akipata. ¹⁶ Munu paalapa, anlapira munu wakunzaidi álavya ushahidi, na kilapo ciwalavya wanu dana.

¹⁷ Basi, Mwenyezimungu kâsaka kuwa ware waja kuriti tamaa yake wejiwe kuwa aapindula vyasemire, ndimana tamaa-yo iye kalapira. ¹⁸ Kwa javyo, julu ya vinu viwiri[†] savipinduriwa, (na novyo avikidirika Mwenyezimungu kulongopa), ofwe tintuwirire iye tirimbisiwa myoyo tikore makono mawiri tamaa ituriwe mbere yetu. ¹⁹ Eyo tamaa-yo iwa kamba nanga ya ngalawa, ítirimbiisa myoyo isiwe na dana isaka kuwa yonse. Kamana tamaa-yo ípita papazira ya nyumba takatifu ya

[‡] 5:11 “Mwaha-wu” ndi kuwa Almasihi vyawere nkulungwa wa dini kamba vyákiwa Melkizideki.

* 6:14 Ona

Mwanzo 22:17. [†] 6:18 “Vinu viwiri” ndi tamaa yaalavire Mwenyezimungu na kulapa kwake.

mbinguni, ikwingira mahala patukufu paari Mwenyezimungu.²⁰ Kweli, epo ndi pengire Insa, kábula ya ofwe, kwa ajili yetu. Kamba vyawere Melkizideki, neye novyo kalawirira kuwa nkulungwa wa dini wa daima milele.

7

Melkizideki nlongozi wa dini

¹ Noyu Melkizideki-yu ákiwa nfalume wa Salemu, na ákiwa nlongozi wa dini akintumika Mwenyezimungu, Nlungu nkulu pakulu. Iye paakiludi Iburahima kuvita yakuwashinda mafalume, kasi-manana naye, akinjanliya.* ² Iburahima, vinu piya vyâapatire kuvita, kálavya fungu rakumi, akimpa Melkizideki. Zina ra Melkizideki mana ake “nfalume wa shariya”. Kwa kuwa ákiwa nfalume wa Salemu, zina rake rkíwa nawo novyo mana ake “nfalume wa usalama”. ³ Iye aawere nawo wawaye wala mamaye, wala aipo waraka ya mazina a wakinya babuze. Ejiwikane mwaka waapongoriwe wala waafwire. Ndimana akilandanisawa Mwana wa Mwenyezimungu, kawa nlongozi wa dini wa milele.

⁴ Onani, Melkizideki vyawere munu bora pakulu! Anta Iburahima, noyo babu yetu nkulu, kâmpa fungu rakumi kwa vinu vyawapokere maaduwi wake kuvita. ⁵ Na ujukulu wa Lawi, ware wâpewe cewo ca ulongozi wa dini, watumiwe nTaureti kupokerera fungu rakumi ra vinu vyawakipatanga wanu walzraeli, wanduzawo, ingawa newo novyo wákiwa ujukulu wa Iburahima. ⁶ Basi Melkizideki, ingawa aawere wa rikolo ra Lawi, kâpokerera fungu rakumi ra Iburahima, na kânjanliya Iburahima, noyo âpokerere tamaa za Mwenyezimungu-*yo*. ⁷ Hapano atikina kuwa ire ajanliya ndi bora koliko ajanliwa. ⁸ Kwa upande wa walongozi wa dini wa rikolo ra Lawi, wâpokerere fungu rakumi wákiwa wanadamu mwinsho wafwa. Fala upande wa Melkizideki, rípokereriwa na munu ari hai, kamba vyaulaviwe ushahidi kuhusu iye. ⁹ Tanawo shariya ya kwamba anta

* 7:1 Ona Mwanzo 14:17-19. † 7:10 Kusema kweli, nowo wakati-wo Lawi ákiwa saanapongoriwa. isema nani ári na haki yakuwa nlongozi wa dini. § 7:13 Kigeregu: “uralu”. * 7:17 Ona Zaburi 110:4. † 7:21 Ona Zaburi 110:4.

Lawi, akipokereranga fungu rakumi noyo, neye novyo kalavya fungu rakumi julu ya Iburahima,¹⁰ kwa kuwa ákiwa mmwiri mwa Iburahima babuye, paasimanane na Melkizideki.[†]

Nlongozi mwengine wa dini, kamba Melkizideki

¹¹ Sambi, ikisakikana kazi ya walongozi wa dini wa rikolo ra Lawi ipate wanu wa Izraeli wafulate shariya yawâpewe. Ináwa ulongozi-wo utimiza ukamilifu, singari kasakikana nlongozi wa dini wa namuna nyengine kamba Melkizideki, sairi wa namuna ya Aruna wa rikolo ra Lawi. ¹² Paatawaziwa nlongozi mwengine wa dini, flazimu shariya neyo novyo ipinduriwe.[‡] ¹³ Kamana Mwenye wetu, ambíwa mMandiko-mu, aawere wa rikolo ra Lawi, na nkati ya rikolo rake tangu aalawirire mmojawapo wakutumika cewo ca nlongozi wa dini[§]. ¹⁴ Aapo atikina kuwa Mwenye wetu kâlawirira kurikolo ra Yuda. Na kuhusu rikolo-ro, Musa aasowere kinu upande wa nlongozi wa dini.

¹⁵ Sambi tikwereriwa sana: kâlawirira nlongozi wa dini namuna nyengine, wakulandana na Melkizideki. ¹⁶ Iye aalawirire kuwa nlongozi wa dini kwa kufulata shariya na shuruti za kufulatana ka rikolo, ila kwa sababu ya uwezo wa mainsha ake seesa tena. ¹⁷ Kweli, Mandiko Matakatifu* ak-wamba:

“Uwe kuwa nlongozi wa dini wa milele kwa namuna ya Melkizideki.”

¹⁸ Basi shuruti ya mida yasiwa konta aina nguvu na aifái kinu, ¹⁹ kamana Taureti aifikamilisha kinu. Fala sambi-pa Mwenyezimungu katisakurira tamaa ngema pakulu ipate julu yake tiwe pamoja naye.

²⁰ Na eyi tamaa-*yi* yakikishiwa kwa kilapo. Pawakitawaziwa walongozi wa dini wengine, Mwenyezimungu aałapire,²¹ fala paalawirire eyu kuwa nlongozi wa dini, Mwenyezimungu kalapa, kamwambira javi[†]:

7:12 Shariya

7:10 Kusema kweli, nowo wakati-wo Lawi ákiwa saanapongoriwa.

7:11 Ona Zaburi 110:4.

7:21

"Omi Mola nñlapa, sipindula kauli yangu. Ukuwa nlongozi wa dini wa milele."

²² Kwa sababu ya kilapo-co, Insa atipa uhakika kuwa eyi miyadi-yi ndi bora pakulu zaida ya mida.

²³ Visitoshe, mida wákiwapo walongozi wa dini wengi wakorire kazi fala mwinsho wafwa, awakidirire kuzidi kukola kazi.

²⁴ Fala Insa kankuinshi kwa milele, na kazi yake ya ulongozi wa dini saupitisaniwa tena. ²⁵ Kwa javyo, iye kanawo uwezo, sambi-pa mpaka milele, wakuwawusha wanu wóka ka Mwenyezimungu julu yake. Kweli, iye kankuinshi daima-zi kuno akiwalebelela nowo wanu-wo.

²⁶ Basi Insa ndi nkulu wa wakulungwa wa dini wakutitendera piya visakikana vyonse. Iye takatifu, aana dambi anta mmoja wala kinu cakunyata, na katanusisa nkati ya madambi mulumwengu-mu akituriwa mbinguni. ²⁷ Iye aari kamba walongozi wa dini wa mida, wakiperekanga kafara daima-zi, cakwanza wakitenda wapate kufutiwa madambi awo wanyewe, ikisa ka madambi a wenziwaho. Fala ka Insa sjavyo! Iye, paaripereke mwanyewe, kalavya kafara mara moja noyo tu basi kwa daima. ²⁸ Nkati ya Taureti, wanu sawakiwa makamilifu wakitawaziwanga kuwa walongozi wa dini. Fala kauli ya kilapo, cilapiwe bandi ya Taureti, katawaziwa Mwanawé, mwenyé kukamilika daima milele.

8

Insa ndi shikarakanzi wa miyadi yanguvu pakulu

¹ Onani, kinu maalumu catiri kwamba ndi kuwa tanawo nkulungwa nkulu wa dini wa namuna-yo, ekare nkono nrirro wa kiti ca Mwenye Nkulu mbinguni. ² Iye áhudumu vitakatifu nkati ya ema takatifu yakweli, saitengiwe na wanadamu, ila Mola. ³ Kila nkulungwa nkulu wa dini ákitondoriwa apereke swadaka na kafara. Ndimana ikilazimu neye awe nawo kinu kimojawapo cakuperekwa. ⁴ Insa, anawepo mulumwengu-mu, aangari kuwa nlongozi wa dini, konta kuno wawapo walongozi wa dini waperéka kafara na swadaka, kamba vyashurutisa Taureti. ⁵ Kazi za-watenda ewo nfano tu basi au kinviria ca

kazi zitendiwa mbinguni. Kwa sababu ya javyo, Musa paawere tayari kujenga ema ya miyadi ya kupatana, kâmbiriwa na Mwenyezimungu javi: "More-more, utende sawa-sawa kamba nfano vyawolo-teriwe kumwango."

⁶ Fala sambi-pa, Insa kagabiziwa kazi bora pakulu koliko wakulungwa wa dini wa mida, kwa kuwa iye ndi mwenyé kupatana kwa miyadi bora pakulu ya kupatana. Ndi javyo konta miyadi-yo yanawo tamaa bora pakulu. ⁷ Kamana miyadi ya kupatana yakwanza, ínawa ikamilika, aikisakikana kutula miyadi myengine ya kupatana kapiri.

⁸ Fala mMandiko Matakativu*, Mwenyezimungu áwasutumu wanu wake javi:

"Wakati uwa karibu wanija kutula miyadi mipyä ya kupatana,
na wanu wa Iziraeli pamoja na wanu wa rikolo ra Yuda.

⁹ Eyo miyadi mipyä-yo aija kuwa kamba yaniturire mida na wababu zavo, paníwalongoze sana-sana, nikiwalavya Miswiri.

Ewo awafulate kamba vyaijisaka miyadi-yo, ndimana awaniyerire, amba ndi Mola.

¹⁰ Basi, eyo ndi miyadi yaníja kutula na wanu wa Iziraeli bandi ya nozo suku-zo, amba ndi Mola.

Shariya zangu nitula nkati ya mawazo awo, nikwandika mmoyo mwawo.

Omi nukuwa Nlungu wawo,
newo wakuwa wanu wangu.

¹¹ Aashubutu munu kufundana na mwenziwe wala kufundana na nduye, kumwambira: 'Mwijiwe Mola', konta piya-wo wakuja kunijiwa, ntoto kamba nkulu.

¹² Nukuja kuwatendera huruma, kuswamii makosa awo, madambi awo sishubutu kukumbukira tena."

¹³ Mwenyezimungu paambire miyadi mipyä, miyadi yakwanza katula kuwa yuluvala. Na kinu culuvare na cisire ciwa karibu yakwasiwa kutumiriwa.

* 8:8 Ona Yeremiya 31:31-34.

Miyadi mipya kwa damu ya Insa

¹ Sambi, kwa kutimiza miyadi yakwanza, wanu wakijuzi wantukuze Mwenyezimungu kwa kufulata shariya zituriwe. Na wakiwa nawo novyo mahala patakatifu mulumwengu-mu, ²Ema Takatifu ítengiwa. Ikiwa na misana miwiri. Nsana wakwanza wakwingirira úkitiwa "Mahala Patakatifu". Nkati-mo múkiwa kandiyeru, meza, pamoja na mikate takatifu*. ³Noyo ema-yo nkati-mo ilumuriwa na pazira. Nkati ya pazira-yo, nsana mwengine úkitiwa "Mahala Patakatifu Pakulu". ⁴Nopo ndi paukiwa uralu wakupambiwa na oru, na "Kashoti ya Miyadi" upande piya wakupambiwa na oru. Nkashoti-mo cikiwapo kiyungu ca oru citaiwa maná, ngombo ya Aruna yaâsipuse Mwenyezimungu, pamoja na maluwawo mawiri a mawe ândikiwe ámuri za Mwenyezimungu. ⁵Julu ya kashoti-yo, víturiwa nfano viyumbe vya utukufu. Mbawa zawo zakunkunjuka zifinika mahala Mwenyezimungu pakiswamii madambi. Kuhusu novi vinu-vi, aipo nafasi sambí-pa yakwerezwa piya.

⁶ Piya-vi pavitengeziwe sana-sana, walongozi wa dini wakingiranga nsana wakwanza wa ema† wakitenda kazi zawo. ⁷Fala nsana wapiri wa ema‡, nkulu wa wakulungwa wa dini iye tu basi ndi akingira. Visitoshe, akingira kila mwaka mara moja basi, akisukula damu ya kafara akapereka ka Mwenyezimungu, anlebele aswamii madambi ake na madambi awakorire wanu kwa sababu ya kutikina. ⁸Kwa piya-vi, Roho Takatifu átolotera kuwa, fíkiwa ema ya miyadi ya mida ingari kutumika, ilanda kuwa njira ýúka Mahala Patakatifu Pakulu ainafunguriwa. ⁹Piya-vi kinyume, namuna yakutifunda vinu vya faida rero-vi. Mana ake ndi kuwa swadaka na kafara za manyama zikilaviwanga ka Mwenyezimungu zire azikidirire kukamilisha myoyo ya wanu wakilavyanga kafara wawenye-wo. ¹⁰Ezi kafara na swadaka zitendiwa-zi zishugulikira vinu vya mwiri basi, kwa nfano, namuna ya kurya, kunywa, na zakuriswafi. Zitumika

mpaka Mwenyezimungu paasaka kutula namuna nyipyä za kuinshi.

¹¹ Fala Almasihi, paalawirire kuwa nkulu wa wakulungwa wa dini kuwa atipe vyema vyajisire, iye kawa ema bora pakulu na yakukamilika kupunda ikiwepo mulumwengu-mu. Ema-yo aitendiwe na wanadamu, mana ake siyo ya mulumwengu-mu. ¹²Iye, pengire mara moja tu basi kwa milele Mahala Patakatifu Pakulu, aasukure damu ya mbuzi wala ya ng'ombe ila kâsukula damu yake iye mwanyewe, apate kutombola milele. ¹³Mida wanu wacafu miri yaho ikiswafi julu ya kutawanyika damu ya mbuzi au ya ng'ombe, na kúpakiwa rivu ra mwana wa ng'ombe wakociwa. ¹⁴Kwa javyo, futi damu ya Almasihi aizidi kutiswafi? Iye, julu ya Roho wa milele, kariperekwa mwanyewe kawa kafara kamili saina baka ka Mwenyezimungu. Damu yake itiswafi myoyo yetu, tase vitendo vitilongoza kukifo, ipate tintumike Nlungu hai.

¹⁵ Kwa javyo, Insa Almasihi ndi mwényé kupatanisa kwa miyadi mipya, ipate irati ya milele Mwenyezimungu yaawapere tamaa ware watondoriwe wapate. Iwapo eyi nafasi-yi konta madambi awo awakorire wakati wa miyadi ya mida womboriwa na kifo ca Almasihi. ¹⁶Sambi, miyadi yakupatana yaaturire Mwenyezimungu iwa kamba waraka yakuritisa. Upande wa noyi waraka-yi, ikibidi kwakikishiwa mwényé kwandika-yo kuwa kafwa. ¹⁷Kweli, waraka yakuritisa aina faida ikiwa andike-yo angari hai, fala bandi ya kufwa andike, waraka-yo yanawo faida. ¹⁸Ndimana ikibidi kuwa ciwepo kifo kimojawapo ipate miyadi iwe na faida. Anta miyadi yakwanza, noyo aitumike bila kutawanyika damu. ¹⁹Mmiyadi yakwanza, Musa pesire kuwambira wanu piya ámuri ya nTaureti, kâtumira minyani ya husopo yakufungiwa na luzi reundu, kâtwala damu ya ng'ombe na ya mbuzi. Ikisa akisulusa na maji, akisasanyira kitabu ca Taureti pamoja na wanu piya, ²⁰akamba§: "Eyi ndi damu ya miyadi yaaturire Mwenyezimungu kwenu umwe." ²¹Na ema ya miyadi-yo, pamoja na

* 9:2 Mikate takatifu ikilawiwanga swadaka ka Mwenyezimungu. † 9:6 "Nsana wakwanza wa ema" ndi "Mahala Patakatifu". ‡ 9:7 "Nsana wapiri wa ema" ndi "Mahala Patakatifu Pakulu". § 9:20 Ona Kulawa 24:8.

piya vinu vikitumiriwa nkati yakuntukuza Mwenyezimungu, Musa kâsasanyira novyo damu.²² Basi, Taureti ikilazimisha kiyasi ca vinu piya viswafiwe julu ya kutawanyika damu. Na ikiwa damu aitawanyike, akupo kuswamiiwa dambi.

²³ Sambi, ikibidi kuwa vyombo vikitumiriwa kuntuza Mwenyezimungu viswafiwe julu ya namuna-yi. Fala evyo mifano tu basi ya vinu vyakweli viri mbinguni. Ndimana vinu vyakweli mbinguni vishurutisa kafara ya faida bora pakulu. ²⁴ Kamana Almasihi engire Mahala Patakatifu pakutendiwa na makono a wanadamu, engire pakulandaniwa nfano tu basi wa mahala pakweli. Aiwere javyo! Kengira mbinguni kawenye, mbere ya Mwenyezimungu, kutitendera fadili ofwe.

²⁵ Na engire kurilavya kafara mara nyingi, kamba nkulungwa wa dini wa Mayahudi vyakingiranga Mahala Patakatifu Pakulu kila mwaka, na damu sairi yake. ²⁶ Inawa javyo, Almasihi akijuji atabike mara nyingi zawenye tangu kumbiwa ka ulumwengu. Kwasa javyo, epa utimiziwa wakati wa mida, ufika wakati wa sambi-wu, iye kolotiwa kwa kuriperekwa kufwa mara moja tu basi kwa milele, alavye mizigo ya dambi. ²⁷ Piya wanu ituriwa wafwe mara moja tu basi, ikisa waje walamuriwe na Mwenyezimungu. ²⁸ Kwa javyo Almasihi, neye novyo kâriperekwa mara moja kuwa kafara alavye dambi za wanu wengi. Ikisa, aktija kwisuka mulumwengu mara yapiri, fala eyo mara-yo, anzima yake siyo kulavya dambi, ila kuwavusha wanu wari kunrindira iye.

10

¹ Kwa kufulata Taureti, wanu wakisaka kuka karibu ya Mwenyezimungu kuntuza wakilavya kafara daima-zi kila mwaka. Fala Taureti tangu-tangu aiwera na uwezo wa kuwaswafi wanu-wo. ² Ináwa nowo wanu-wo kweli-kwelini waswafiwa nfululu, awangari kurifahamu tena kuwa na madambi, ndimana singari isakikana kuludira tena kutenda kafara, sinovsky? ³ Fala kusema kweli, nozo kafara-zo zankuwatenza wanu kukumbukira dambi

zawo kila mwaka. ⁴ Konta damu ya ng'ombe na ya mbuzi aina uwezo wa kulavya dambi.

⁵ Kwa javyo, Almasihi, pengire mulumwengu-mu, kasema ka Mwenyezimungu*:

“Ausakire kafara wala swadaka, ila kunitengeza mwiri.

⁶ Azukwajibu kafara za nyama wakociwa, wala swadaka ipate uswamii madambi.”

⁷ Ikisa Almasihi kamwambira Mwenyezimungu:

“He Mwenyezimungu, niwa epa kutimiza nafsi yako, kamba vyavyandikiwe kuhusu omi nkitabu ca Mandiko.”

⁸ Basi Almasihi, bandi yakusema:

“Ausakire na azukwajibu kafara za manyama wakociwa, wala swadaka zakulaviwa kupata kuswami-iwa madambi”

(ingawa ezi kafara-zi zilazimishiwa nkati ya Taureti), ⁹ kamwambira Mwenyezimungu: “Niwa epa kutimiza nafsi yako.” Basi, Almasihi kafuja miyadi ya mida[†] katula miyadi yapiri‡. ¹⁰ Kwa noyo nafsi-yo, julu ya swadaka ya mwiri wa Insa Almasihi mara moja kwa milele, ofwe titakatifwiwa.

¹¹ Kila nlongozi wa dini awahudumu Mayahudi kila suku ákikola kazi, ákiperekwa kafara namuna moja noyo mara nyingi zawenye. ¹² Falakini Almasihi kârilavya iye mwanyewe akiriperekwa kuwa kafara kwa mara moja noyo tu basi, kafara-yo ífái milele. Ikisa kekala mahala bora pakulu, upande wa nkono nriro wa Mwenyezimungu. [§] ¹³ Tangu nopo kankurinda mpaka Mwenyezimungu awature maaduwi wake kumaulu kwake.* ¹⁴ Basi iye, kwa kuriperekwa mara moja noyo tu basi, ware waawatenza utakatifu kawatula ukamilifu kwa milele. ¹⁵ Na kinu-ci Roho Takatifu neye katakikisha, kanza kutereza usemi wa Mola asema javi†:

* 10:5 Ona Zaburi 40:6-8. † 10:9 Kafuja miyadi ya mida pamoja na tabiya yakulavya kafara-yo. ‡ 10:9 “Miyadi yapiri” ndi kafara nyipya ya Insa mwanyewe. § 10:12 Ona Zaburi 110:1. * 10:13 Ona Zaburi 110:1. † 10:15 Ona Yeremiya 31:33.

¹⁶ “Bandi ya nozo suku-zo, eyi ndi miyadi yanjáa kuwaturira ewo, amba ndi Mola. Shariya zangu nitula mmyoyo mwawo, nikwandika nkati ya mawazo awo.”

¹⁷ Ikisa kaamba javi‡:

“Madambi awo na makosa awo sishubutu kukumbukira tena.”

¹⁸ Onani, madambi-yo paaswamiiwe, aisakiana tena swadaka nyengine yakufuta.

Tukeni tiwe karibu ya Mwenyezimungu

¹⁹ Sambi, wanduzangu, tanawo uhakika wakwingira Mahala Patakatifu Pakulu julu ya damu ya Insa, ²⁰ njira nyipya ya uhai katifungurira julu ya kupapula pazira paapereke mwiri wake. ²¹ Ndi kweli novyo kuwa tanawo nlongozi wa dini nkulu pakulu, amiri wa nyumba ya Mwenyezimungu mbinguni. ²² Kwa javyo, tukeni tiwe karibu ya Mwenyezimungu na myoyo ya ukweli na kwamini nfululu, tiwe na myoyo yakosiwa fahamu mbaya na miri yetu yakoziba na maji swafi. ²³ Tamaa yatereziwe, tukeni tizidi kutumaini bila dana, konta Mwenyezimungu alavire tamaa mwaminifu.

²⁴ Tukeni tiwaze namuna zakushongana pendo na vitendo vyema. ²⁵ Tisitowe, kamba tabiya za wanu wamojawapo, kuka kujumana na wenzetu kujamatii. Kwasa javyo, tukeni tirimbisane myoyo kila mara, konta mukwijija kuwa suku ya Kiyama iwa karibu.

²⁶ Kamana bandi yakwereriwa ukweli sana-sana na kukubali, tikilangela kuzidi kukola dambi, basi aipo kafara anta moja yakufái kutiswamii madambi. ²⁷ Ila ka wabishi, ciwabakire kinu kimoja basi, kurindira na wofi nkulu hukumu ya Mwenyezimungu na kulungula moto mwangi wakofya. ²⁸ Mida munu akikatala kufulata Taureti yéusiriwe Musa, wakilawirira mashahidi wawiri wakwakikisha kuwa kakosa akihukumiwa kifo, aakiwoneriwa utungu. ²⁹ Fikirini ndi hukumuni ulu iwapata wanu wakunkejeli Mwana wa Mwenyezimungu! Ware sawatula ubora

damu ya Insa yakkakikisha miyadi ya kupatana iswamii dambi yake! Novyo, wakejeli damu ya miyadi itiswafire, na wafezeyi Roho Takatifu atolotera rehemaa! ³⁰ Kamana tikwijiwa kuwa Mwenyezimungu nkati ya Mandiko Matakatifu§ kaamba javi:

“Kuriripira kwangu; omi niriripirira.”

Na mahala pengine mMandiko, yandikiwa javi:

“Mola awalamula wanu wake.”

³¹ Kugwirira makono mwa Nlungu hai ndi kinu cakofya pakulu!

³² Wazani suku zipitire bandi yakupata nuru ya Mwenyezimungu, muhitamili tabu nydingi zawenye. ³³ Umwe kati yenu, wamojawapo watukaniwa pawanu na watabishiwa, na wengine wakisan-ganyika na watabishiwe ware, newo novyo watabika. ³⁴ Mutabika pamoja na wafungwa, na pavitwariwe vinu vyenu piya, muhitamili hasara na furaha, kwa kuwa mukijija kuwa mukuja kupata vyema pakulu vyakuwepo daima. ³⁵ Basi, musase kurimba moyo konta kukujsiranji tuzo rikulu. ³⁶ Kamana mujuzi muhitamili kwa imani mutimize nafsi ya Mwenyezimungu, ipate mupokerere vire vyakupereni tamaa. ³⁷ Konta mMandiko*, Mwenyezimungu akwamba:

“Ubaki wakati aba futi wakuja ire akirindíriwa, aakáwa.

³⁸ Fala kamilifu wangu áinshi julu ya kwamini†.

Saanihitamili, siri radi naye.”

³⁹ Ofwe atiri kamba ware sawahitamili wakupoteya, ila tintumaini Mwenyezimungu, ndimana tívushiwa.

11

Namuna zakuntumaini Mwenyezimungu

¹ Sambi, “kwamini” mana ake ndi kuwa nawo uhakika wakuwa na tamaa ya vinu saviwoneka viri vyakweli. ² Kamana julu ya kwamini, wababu zetu wa mida wajibisa ka Mwenyezimungu.

‡ 10:17 Ona Yeremiya 31:34. § 10:30 Ona Kumbukumbu 32:35-36. * 10:37 Ona Habakuki 2:3. † 10:38 Ona Habakuki 2:4; waRoma 1:17; waGalata 3:11.

³ Julu ya kwamini, tikwereriwa kuwa wasaa umbiwa julu ya usemi wa Mwenyezimungu, vinu vyakuwoneka vyumbiwa na kinu saciwoneka.

⁴ Julu ya kwamini, Abeli kalavya kafara ngema zaida ya Kaini, ndimana kajibisa ka Mwenyezimungu kuwa kamilifu. Mwenyezimungu kolota kuwa kawa radi naye julu yakupokerera kafara yake. Ingawa iye kâfwa, fala julu ya kwamini kwake, angari akisowera.

⁵ Julu ya kwamini, Henoki katwariwa kaperekwiwa mbinguni, iye aafwire. Hapana munu ammonire tena konta Mwenyezimungu kantwala. Kâbula yakutwariwa mulumwengu-mu, kâjibisa ka Mwenyezimungu. ⁶ Aashubutu munu kwajibisa ka Mwenyezimungu bila kuntumaini iye. Konta asakúla kuka upande wa Mwenyezimungu ájuzi atumaini kuwa iye kawapo na awatuza wenyewe kuka upande wake.

⁷ Julu ya kwamini, Nnu kâsikiriza sana-sana paambiriwe na Mwenyezimungu kuhusu vinu savikiwoneka vîkija kukuna mbere. Kwa kumwinshimu Mwenyezimungu, kalunda safina invushire iye pamoja na jamaa zake. Kwa namuna-yo, Nnu kâlamula kuwapa hukumu wanu wa mulumwengu-mu. Novyo, kâriti ukamilifu wakulawirira julu ya kwamini.

⁸ Julu ya kwamini, Iburahima kâsikiriza paamuriwe kusama, kuka inti nyengine yaampere tamaa Mwenyezimungu kuwa akuja kuriti. Kôka ingawa aakijiwa mahala kaakuka.

⁹ Julu ya kwamini, akiinshi kamba malamboni inti yaâmpere tamaa Mwenyezimungu. Iye ákikalanga muema pamoja na Izaki na Yankubu, wenyewe kuriyi sawa-sawa cire caâwpare tamaa Mwenyezimungu.

¹⁰ Iburahima akirindira kwikala kaya ya aliserusu yakukomala, yaapangire na yaajengire Mwenyezimungu mwanyewe.

¹¹ Julu ya kwamini, Iburahima kâpata uwezo wa kumpongola mwana. Ingawa kôluvala pakulu na nkawake Sara aakipongola, kâkidiri konta akitumaini kuwa Mwenyezimungu kamilifu, atimiza tamaa yake. ¹² Kwa javyo, julu ya munu mmoja, noyo ári karibu kufwa, ulawirira ujukulu mwiningi wawenye, kafyala-kafyala kamba

nondwa za mbinguni au kamba misanga ya mwani.

¹³ Julu ya kwamini, ewa wanu-wa piya wafwa wakitumaini, bila kupata kinu cawapewe tamaa, fala mmoyo wakiwona na wakisheherekera baidi, na wakikisha kuwa inti ire aiwera yavo, ila ewo wanu wakupita mulumwengu-mu. ¹⁴ Wakiséma javyo kolota kuwa wankusakula inti yavo wanyewe. ¹⁵ Inawa wakiwaza kuhusu inti yawâlawire, nanga wapata nafasi kulidira noko. ¹⁶ Fala kwasa javyo, ewo wakiwa nawo hamu kufika inti ngema pakulu, inti ya mbinguni. Ndimana Mwenyezimungu aawona haya kwitiwa Nlungu wawo ewo. Kusema kweli, iye kawatengezera kaya yavo.

¹⁷ Julu ya kwamini, Iburahima paay-ereriwe, ákiwa tayari kunlavya mwanawee Izaki awe kafara. Ire waâpewe tamaa, kanleva kuwa kafara mwanawee mmoja noyo tu basi, ¹⁸ ingawa kâmbiriwa mida kuwa: "Julu ya Izaki ndi kauja kulawirira ujukulu wako."

¹⁹ Iburahima kamini kuwa Mwenyezimungu ákiwa na uwezo wakunludisira uhai anta afwe. Na ka ukweli, kinyume, ilanda kam-pokerera afwire futi.

²⁰ Julu ya kwamini, Izaki kâwajanliya kuhusu mambo akija kuwakuna mbere wanawee Yankubu na Ezau.

²¹ Julu ya kwamini, Yankubu, suku aba kâbula yakufwa, kâwajanliya wana wa Yusufu mmoja-mmoja. Neye akimwabudu Mwenyezimungu kuno enyamire nkongojo wake.

²² Julu ya kwamini, Yusufu paawere karibu kufwa, kâkumbukira tamaa yakuwa ujukulu wake ukuja kulawa Miswiri uludira kwavo. Ndimana kâwalaizira wanawee vyawakijuzi kutenda makongo ake.*

²³ Julu ya kwamini, wawaze Musa, bandi yakumpongola mwana wawo, wanfisa kwa muda wa myezi mitatu. Wâmmona toto ire kuwa mwema pakulu na kwa sababu ya kwamini kwavo, awopire shuruti ya nfalume.

²⁴ Julu ya kwamini, Musa paakurire, kâkatala kutukuziwa kamba munu bora pakulu kwa sababu ya kuwa njukuluwe Firyauna nfalume wa Miswiri. ²⁵ Kwake iye kawona kuwa vyema pakulu kutabika

* 11:22 Kâwambira kuwa suku moja walziraeli wakúja kulidira kwavo, ndimana wajuzi wasamise makongolo ake.

na wanu wa Mwenyezimungu koliko kufurahira mambo a dambi kwa muda aba.²⁶ Iye akiwaza kuwa kutabika kwa kufezeyiwa kamba vyaja kutabika Almasih, ndi bora pakulu koliko mali piya a Miswiri. Akiwaza javyo konta akirindira kupata tuzo mbere.

²⁷ Julu ya kwamini, Musa paalawire Miswiri opire kukimiwa ka nfalume. Kahitamili kamba ari kummona ire sawoneka[†].

²⁸ Julu ya kwamini, Musa kâwambira walziraeli wasasanyire damu mmiryango mwawo ipate Mwenyezimungu, paasaka kuntuma Nzulairi kuwolaya wana watanzi wa WaMiswiri, asiwolaye wana watanzi wa walziraeli.

²⁹ Julu ya kwamini, walziraeli wâloka Bahari Nyendumu, wapita kati-kati ya bahari pakukama maji. Fala waMiswiri, pawakenkeze kutenda novire, wazama, wafwa piya.

³⁰ Julu ya kwamini, ukuta wa Yeriko bandi ya kuzunguriziwa muda wa suku saba, ûgwa.

³¹ Julu ya kwamini, reba wakwitiwa Rabhu kâwapa mamburo manasonde wa Izraeli, ndimana aafwire pamoja na ware sawakinsikiriza Mwenyezimungu.

³² Mwaja, musaka nukwambireni kinani tena? Wakati uniwera aba, nanga nukwambirani kuhusu Gidiyoni, Baraki, Samsoni, Yefta, Daudi, Samuweli, pamoja na minabii wengine. ³³ Ewo, kwa kuwa wâmwamini Mwenyezimungu, wâwashinda mafalume wengine, wâtimiza shariya ya Mwenyezimungu, na wâpata Mwenyezimungu vyawapere tamaa. Awawasire masimba kuwaduru,³⁴ wâzimisa moto mwingu wawenye, wakinusurika mmakono mwa ware wakisaka kuwolaya na mapanga. Ingawa wâveya, wâlawirira kuwa na nguvu, wâlawirira kuwa masurudadu wakofya mpaka wâwashinda masurudadu wa inti nyengine.³⁵ Wanawaka wakifwiriwa fala kwa kumwamini Mwenyezimungu wâwapokerera wafwi walo, wafwi-wo waludira uhai.

Wanu wengine, kwa kunfulata Mwenyezimungu, wâkatala kufunguriwa nkalambo, ndimana wêbiwa mpaka kufwa. Watenda javyo ipate waludisiriwe uhai

wapate mainsha meema pakulu.³⁶ Wengine wâtabika na matusi na kukonyoriwa, wengine wâfungiwa na alucema na wâtaiwa nkalambo. ³⁷ Wengine wâkipanjiwa na mawe mpaka kufwa, wengine wâkibaluriwa kati-kati, wengine wâkulaiwa na upanga. Wengine wâkenenda wakisamasama, wakivalanga masambala a kondoo au a mbuzi, newo wâkiwa wakosofu pakulu, wakitabishiwa na wakopepesiwa.³⁸ Wanu-wo ulumwengu-wu auwajuzire. Wâkipayapaya nlanga na mmyango, wakiinshi mmajonga na mmapondo kamba wanu wakutíra.

³⁹ Wanu ware piya, ingawa wâjibisa ka Mwenyezimungu kwa kwamini kwavo, fala novyo-sivyo, awapokerere vyawapewe tamaa.⁴⁰ Evi vikuna konta Mwenyezimungu katipangira kinu cema, kuwa bila ofwe, wasikamilike.

12

Mwenyezimungu ndi Baba wetu

¹ Sambi, kwa kuwa tizunguriziwa na kundi ra mashahidi, tukeni tase piya vitendo vitikataza vyatijuzi kutenda, tase dambi iri kutiziwiriza pakulu. Tukeni tituwirire kwa kuhitamili njira ituriwe mbere yetu ofwe. ² Tukeni tizidi kunnang'aniza Insa, kulongoza kwamini kwetu, tangu mwanzo mpaka mwinsho. Iye kahitamili kutabika pansalaba, aimmwereire aibu, kwa sababu ya radi ituriwe mbere yake. Epa sambi kekala mahala bora upande wa nkono nriro wa kiti ca Mwenyezimungu.

³ Aye, tunzani sana-sana kuhusu iye, kawavumírica pakulu wamâdambi wakin-tendera husuma, ipate musikore, wala isukulaweni niya. ⁴ Kamana vita yenu yakubishana na dambi, amunamba kufika wakati wa kuvumírica mpaka wanu waku-ulyen. ⁵ Kwasa javyo, amukumbukira usowezi urimbisa moyo? Muriwala caak-wambireni Mwenyezimungu konta umwe muwa wanawe? Mandiko Matakatifu* ak-wamba:

“Mwanangu, fikiri sana-sana Mola paakolotera makosa ako.
Iye paakusutumu, usiuzunike.

[†] 11:27 “ire sawoneka” ndi Mwenyezimungu.

* 12:5 Ona Ayuba 5:17; Usowezi 3:11.

⁶ Konta Mola awolotera makosa ware waawapenda.

Piya waawapokerera kuwa wanawe, iye ndi wawasútumu[†].

⁷ Ndimana Mwenyezimungu paakusutumuni, vumirirani. Mwenyezimungu akuwonani kamba wanawe. Na kweli, mwanani sasutumu na wawaye?

⁸ Wasimana piya wásutumiwa. Ndimana, ikiwa aakusutumireni, ilanda kamba mwana wakunsingana, ailanda kamba muwa wanawe wakweli. ⁹ Visitoshe, wawa zetu mulumwengu-mu watisutumu na ataswa kuwasifu. Futi ofwe atinsikiriza Baba wetu wa mbinguni tipate kuinshi vyema?

¹⁰ Wawa zetu mulumwengu-mu watisutumu kwa wakati aba, kwa ngano zavo zawa wona kuwa ngema. Fala Mwenyezimungu atisutumu kwa vyema vyetu wanyewe, ipate tiwe watakatifu tinlande iye. ¹¹ Basi, mulumwengu-mu kila mara patisutumiwa pone, tívona kuwa kitendo cakutipa uzuni, acitifuraisha mmyoyo mwetu. Fala wapatire kusilimuka kwa kusutumiwa na Mwenyezimungu, mwinsho wápata thawabu ya kuinshi kwa ukamilifu na usalama.

¹² Kwa javyo, lamukani muririmbise murolore muwe na nguvu. Rimbisan malundi enu mepepe-wo, musiteteme!

¹³ Enendani njira yakoloka ipate musizidi kuremala, ila mupone.

Musiture minyongo rehema ya Mwenyezimungu

¹⁴ Sakulani namuna za kuinshi kwa usalama na wanu piya na nshugulikireni Mola, konta saanatenda javyo, aakidiri kummona. ¹⁵ Rikengereni musiture minyongo rehema ya Mwenyezimungu. Rikengereni, nkati yenu asilawirire munu wakuwa na sumu kamba utupa, kuwatenza wenzwi wengi kwingira haramu.

¹⁶ Rikengereni nkati yenu asilawirire munu sharati, au kamba vyawere Ezau, saana inshima na vinu takatifu. Iye, kwa kupata finga moja tu basi ya cakurya, kâperekha haki yake ya utanzi kupongoriwa.

¹⁷ Mukwijiwa kuwa mwinsho kadai haki yajanliiwe na wawaye, fala kâkataririwa. Aakidiri kopindula vyaâtendire, ingawa

kasakula haki yake kuno akinlawa masozi mengi.

¹⁸ Umwe ámuri kamba walziraeli wâfikire karibu ya Mwango wa Sinayi ukilawa malulimi a moto. Newo ûfinikiwa kupi na giza, kuno mepo ikivunga thi-thi,

¹⁹ baramanda ikivuma, na shauti ya Mwenyezimungu ikisowera mpaka wakin-tafadali wakamba: “He! Atikidiri kusikira tena usowez i wake!” ²⁰ Ewo awâkidirire kuhitamili ámuri ya Mwenyezimungu ikisema javi[‡]: “Munu au ndudu asaka kukumbula mwango ure onse apanjiwe na mawe mpaka afwe.” ²¹ Víkunire kuMwango wa Sinayi, anta Musa noyo vímopepesa, akamba[§]: “Nankutetema, wof!”

²² Fala umwe mufika karibu ya Mwango wa Ziyoni na Yerusalem ya binguni, kaya ulu yekala Mwenyezimungu hai, mahala kawari malaika laki-ka-malaki.

²³ Mufika kujamati ya wana wakwanza kupongoriwa*, mazina awo andikiwe mbuku paandikiwe mazina a ware wóka mbinguni. Mufika karibu ya Mwenyezimungu, mwenyé kuwalamula wanu piya. Mufika novyo karibu ya roho za wanu wa shariya walawirire sambi kuwa makamilifu.

²⁴ Epa, mufika karibu ya Insa, mwenyé kupatanisa kwa miyadi mipya. Mufika karibu ya damu yake itawanyike, iri na uwezo pakulu zaida ya damu ya Abeli.

²⁵ More-more, musikatare kunsikiriza ári kusowera! Kamana, ikiwa ware wakatare kunsikiriza Musa apereke habari za Mwenyezimungu, awanusurike kuhukumiwa, futi ofwe! Tikuja kuhukumiwa pakulu, tikintula minyongo Mwenyezimungu asowéranofwe binguni! ²⁶ Wakati wa Musa, shauti ya Mwenyezimungu itetemesa ardhi, fala sambi Mwenyezimungu katipa tamaa nkati ya Mandiko javi:

“Nitetemesa inti tena, wala si inti basi, na bingu neyo novyo.”

²⁷ Sambi, usemi wa “tena” utolotera kuwa vinu vyumbiwe vyonse vitetemisiwa na vilainika, ila vibaki ndi vire savitishiwa. ²⁸ Basi, kwa kuwa tipokerera ufalume savitishiwa, tishukuru. Kwa javyo, tintumike Mwenyezimungu kwa namuna zakumwajibu iye, kwa kumwinshimu na

[†] 12:6 Ona Usowez 3:12. [‡] 12:20 Ona Kulawa 19:12-13. [§] 12:21 Ona Kumbukumbu 9:19.

* 12:23 “Wana

wakwanza kupongoriwa” ndi wenye kwamini.

kumopa. ²⁹ Kamana Nlungu wetu kawa kamba moto nkali vyaupoteza.

13

Namuna za kumwajibu Mwenyezimungu

¹ Kamba munu na nduye, zidini kupendana. ² Musase kuwakaribisha wayeni, konta kwa kutenda javyo, wamojawapo wafikirira kuwapokerera malaika mmanyumba mwawo bila kwijiwa.

³ Watendereni huruma wanu wafungiwe na muwasaidiye, onani kamba mufungiwe nawo pamoja. Watendereni huruma wanu wari kutabika, tulani kamba utabika mwiri wenu pamoja newo. ⁴ Wanu piya wajuzi wainshimu ndowa. Kusema kweli, muka na nlume wenarirane, kamana Mwenyezimungu akúja kuwahukumu wazinzi pamoja na masharati. ⁵ Vinu vyakuuziwa na nzuruku, zidini kutowa kuperereza. Vikutosheni vinu vyamuri nawo, kamana Mwenyezimungu kasema: "Sukwasa futi, wala sukutipuka." ⁶Ndimana na hakika tikwamba javi*:

"Mola ndi anisaádiya, omi sopa kinu. Mwanadamu anitenda kinani cakunyata?"

⁷ Wakumbukirenzi wakulungwa wenu wâkwerezeni habari za Mwenyezimungu. Tunzani vyawainshire na vyawafwire. Wafulatizeri kwamini kwawo. ⁸ Insa Almasihi ndi mmoja noyo, ijana na rero na milele-*yi*. ⁹Musiwasikirize wanu wafunda inlimu nyengine jisijisi wakupotezani njira ya ukweli. Císáka kukupani nguvu mmyoyo myenu siyo shuruti kuhusu camujuzi kurya. Kwa kufulata nozo shuruti-*zo*, tangu hapano munu apatire faida yake. Ila cisaka kukupani nguvu ndi rehema za Mwenyezimungu. ¹⁰ Walongozi wa dini wákitumikanga muEma Takatifu ya Mayahudi awana haki ya kurya vilaviwa kafara yakutuku[†] mahala petu pakwambudu. ¹¹Nkulungwa wa dini mara moja kila mwaka[‡] ákisukulanga damu ya manyama, akiperekwa ka Mwenyezimungu Mahala Patakatifu Pakulu, iwe kafara ya kufuta madambi. Fala mwiri wa nozo

nyama-zo úkociwanga panja ya kaya ulu ire. ¹² Ndimana Insa, kwa ajili ya kuwaswafi wanu madambi julu ya damu yake, neye novyo kâfwa panja ya kaya ulu.

¹³ Basi, tukeni tikawe pamoja naye panja ya kaya ulu-*yi*[§], tiwe tayari kukejeliwa kamba vyaakekeliwe iye. ¹⁴ Kamana mulumwengu-mu, atina kaya ya milele, fala tfrindira kaya yatija kuwa nawo mbere.

¹⁵ Basi, julu ya Insa, daima tilavye kafara ka Mwenyezimungu kwa kuntukuza, kwa kwakikisha zina rake na kanywa zetu. ¹⁶Fala musiriware kutenda meema na kumera, kamana ezo ndi kafara zakumwajibu Mwenyezimungu.

¹⁷ Wasikirizeni wakulungwa wenu kwa kufulata ámuri zavo, kamana ewo washugulikira daima faida zenu, wakijiwa kuwa wajuzi kujibu ka Mwenyezimungu. Waseni watende kazi kwa radi. Musiwa-tenze kwisa moyo, kontajavyo aiwepo faida kwenu umwe.

¹⁸ Musase kutilebelela duwa. Tanawo uhakika kuwa myoyo yetu iwa swafi, konta tísakula kutenda meema kwa kila hali. ¹⁹ Visitoshe, nukulebelani ka moyo wangu piya, munilebelela duwa ipate Mwenyezimungu aniludise niwe pamoja namwe kwa suku karibu.

Duwa ya mwinsho

²⁰ Sambi, Mwenyezimungu mwenyé usalamu, anfufure ka wafwi Mwenye wetu Insa, Nsunga nkulu wa makondoo, julu ya damu yakikisha miyadi ya milele, ²¹nínlebelia akupeni piya vinu vyemavyema mutimize nafsi yake, mukitenda vyavimwajibu iye, julu ya Insa Almasihi. Iye atukuziwe daima milele! Aamina.

Masemo a mwinsho

²² Wanduzangu, nukutafadalini mupok-erere ewu usowezí-wu kwa radi kamana nukwandikirani kwa usemi aba.

